## BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Pili – Tarehe 29 Machi, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### MASWALI NA MAJIBU

**Na. 16**

***Master Plan* ya Maji Dodoma**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kati ya kazi nzuri zilizofanywa na Mamlaka ya Ustawishaji Makoa Makuu Dodoma ni pamoja na kutayarisha *Master Plan* ya ujenzi wa Makao Makuu ya Serikali:-

(a) Je, mpango huo kabambe umeathiriwa kwa kiwango gani kutokana na kukiukwa mara kwa mara kwa utekelezaji wa mradi huo?

(b) Je, Serikali haioni kuendelea na ujenzi wa majengo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzani nje ya eneo lililotengwa kwenye *Master Plan* kunaleta dosari kwenye mpangilio mzima wa *Master Plan* na kuyanyima majengo yenyewe nafasi ya kutosha, mandhari na hadhi yanayostahili majengo ya Bunge lolote lile.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Maendeleo wa Mji Mkuu yaani *National Capital Master Plan* uliidhinishwa na Serikali mwaka 1976 na unatoa dira, mwelekeo na maelekezo kuhusu uendelezaji wa Mji wa Dodoma ili ufikie hadhi ya kuwa Mji Mkuu wa Tanzania. Mpangilio wa shughuli zote ikiwa ni pamoja na miundombinu, majengo na huduma zote zinazohitajika vimebainishwa. Hata hivyo, maamuzi ya nini kifanyike hubadilika kwa kuzingatia mazingira yaliyopo, mahitaji ya wakati huo, nyezo zilizopo na mtazamo wa wakati huo. Hii ikiwa na maana kwamba kila zama zina kitabu chake. Aidha, mipango ya Maendeleo ya Miji inapaswa kupitiwa kila baada ya miaka kumi (10) na kuirekebisha ili iendane na hali halisi na mahitaji ya maendeleo ya wakati husika.

Sheria ya Mipango miji ina maelekezo bayana na namna ya kufuta, kurekebisha au kubadilisha kipengele au eneo lolote la mpango. Mchakato mkubwa wa mapitio ya Mpango Kabambe uliofanywa mwaka 1988, ulirekebisha mtazamo, sera, taratibu na hata mpango wa matumizi ya ardhi wa Mpango Kabambe na sasa mpango huo unatumika kwa pamoja na ule wa mwaka 1976 kuongoza maendeleo ya Mji wa Dodoma. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kimsingi Mpango Kabambe haujaathirika na mabadiliko yaliyofanyika yameuboresha na kuufanya uende na wakati.

(b) Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ukumbi mpya wa Kisasa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la *Central Business Park* ulizingatia ushauri wa kitaalamu ambao ulijikita katika matumizi bora ya miundombinu iliyokuwa imejengwa sehemu hiyo na uwezo mdogo wa Serikali kuweza kumudu gharama za ujenzi mpya wa ukumbi wa Bunge na ofisi zake katika eneo tofauti na hapo. Katika eneo hilo la Bunge lilikuwa lina majengo yanayotumika ambayo yameigharimu Serikali kiasi cha Tshs. Bilioni tisa. Eneo hilo tayari lilikuwa lina miundombinu ya barabara na mifereji ya maji ya mvua na maji machafu.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kisheria na kitaalamu zilifuatwa kabla ya usanifu na ujenzi na upanuzi wa Bunge kuanza. Maamuzi haya yalikuwa sahihi na hatua iliyofikiwa ni ya kujivunia kwa kuwa Bunge letu tukufu kwa kipindi kirefu kijacho litakuwa na ukumbi na ofisi za kutosha kuliwezesha kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kijamii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni kwa mamlaka zote husika kuhakikisha kwamba ujenzi katika maeneo yanayopakana na viwanja vya Bunge unafanywa kwa kiwango chenye hadhi ya kulingana na ile ya eneo la Bunge na si vinginevyo.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, na namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri, nina swali dogo tu la nyongeza, nalo ni:

Je, Serikali iko tayari kutoa ahadi ya kwamba kwenye bajeti inayofuata na nyingine zote zitakazofuata baada ya mwaka huu, kwamba Serikali itatenga fedha za kutosha kuiwezesha mamlaka ya ustawishaji wa Makao Makuu kutimiza majukumu yake. Majukumu yake ni pamoja na kuhakikisha kwamba mipango ya mji wa Dodoma inapitiwa mara kwa mara na pia kuhakikisha kwamba majukumu mengine yote ambayo yanaendana na ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma yanatimizwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika kikao cha Bunge lililopita Mheshimiwa Rais wa nchi hii alitamka rasmi kwamba kuanzia sasa uhamiaji wa Wizara mbalimbali kuja Dodoma, utafanywa kufuatana na uwezo wa Serikali. Kwa maana ya kwamba kila tutapokuwa tumepata kiasi cha pesa tutahamisha Wizara zetu na hatimaye kuhakikisha kwamba tunahamia Dodoma. Kwa hiyo ni wazi msukumo wa kutenga pesa kwa ajili ya huduma za ujenzi wa Makao Mkuu utakamilika. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba *Master Plan* haikuathirika, lakini kwa miaka matatu iliyopita hakuna mwaka hata mmoja zimetengwa zaidi ya shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kuendeleza *Master Plan* hiyo, nayo ni kwa kazi ndogo ndogo kama maua na mapambo.

Je, Waziri atakubali kwamba sasa wakati umefika wa kuunda kasma maalum ambapo fedha zitatengwa kwa ajili ya kuendeleza Makao Makuu kuliko ilivyo sasa ambapo fedha zinatengwa ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, majibu mazuri ambayo yametolewa na Naibu Waziri yameeleza vizuri sana nini hatua zinafanyika. Lakini *whether* unakifungu maalum kimewekwa peke yake au kifungu hicho kipo katika usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu hili halileti tofauti. Mimi nafikiri sasa kuna ufanisi zaidi kwa sababu kifungu hicho kikikaa chini ya Waziri Mkuu, na Waziri Mkuu ndio msimamizi wa shughuli za Serikali, kazi inafanyika kwa wepesi zaidi na ufanisi zaidi. (*Makofi*)

Na. 17

**Gari la Kituo cha Afya Magugu**

**MHE. OMAR S. KWAANG' (k.n.y MHE. DAMAS P. NAKEI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kituo cha Afya Magugu ni muhimu sana kwa ukanda mzima wa Tarafa ya Mbungwe na kiko umbali wa kilomita 30 kutoka Hospitali ya wilaya ya Babati; na kwa kuwa kituo hicho kinahitaji usafiri wa uhakika kwa wagonjwa:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa kituo hicho hakina gari (*ambulance*) la uhakika kwa Wagonjwa?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani hadi sasa katika kutoa huduma stahili ya *ambulance* kwa kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spi,a, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Paschal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye sehemu (a) (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la ukosefu wa gari maalum au la uhakika la kubeba wagonjwa, *ambulance*, katika kituo cha afya cha Magugu. Kuanzia mwaka 1996, Kituo hicho cha Afya kilikuwa kinatumia gari aina ya *Land Rover* 109, kwa ajili ya matumizi ya *ambulance.* Kutokana na uchakavu wa gari hilo ambalo limekuwa likiharibika mara kwa mara, Halmshauri ya Wilaya ya Babati iliamua kuanzia mwezi Oktoba 2005 kwamba gari hilo lisitumike tena.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kukosa gari la kubeba wagonjwa, *ambulance*, Halmashauri ya Wilaya ya Babati imeamua kutumia gari la Utawala la Hospitali ya Wilaya, aina ya *Toyota Land Cruiser (Hard Top*) kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri katika kituo cha Afya cha Magugu, pamoja na kubeba wagonjwa, kuwasafirisha wataalam wa afya wanapotekeleza utoaji wa huduma za Kliniki za Mkoba yaani *Mobile Clinic*. Utaratibu unaotumika wa kupeleka wagonjwa ni kuwasiliana na Uongozi wa Wilaya.

Aidha, kuna mtandao wa *radio calls* zilizoko kwenye Zahanati mbalimbali ambapo kukiwa na tatizo zinawasiliana moja kwa moja na hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati ni uamuzi wa busara kwani unakiwezesha kituo hicho kutekeleza majukumu na shughuli mbalimbali za utoaji wa huduma za afya na usafirishaji katika kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeliona tatizo la magari ya kubeba wagonjwa katika vituo vya afya na si kwa Magugu peke yake bali nchi nzima. Hivyo, katika mwaka 2005/2006 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeanza kununua magari kwa awamu kwa Mwaka huu ofisi yetu itanunua magari 25 kwa gharama ya shilingi *bilioni*1.5. Magari hayo yakishanunuliwa yatagawanywa kwa kuangalia baadhi ya vigezo, kama vile Halmashauri zilizoanzishwa hivi karibuni, zile Halmashauri ambazo zina matatizo makubwa ya magari ya wagonjwa, vituo vya afya ambavyo viko mbali sana na hospitali za wilaya, na kuangalia ukubwa na mahitaji ya gari katika eneo husika. Utaratibu huu utaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la gari sasa katika kituo cha afya Magugu ni pamoja na kushirikiana na utawala.

Je, Mheshimiwa Waziri anaamini kwamba sasa tatizo hilo ndio litakuwa limekwisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama kituo cha afya cha Magugu kita *meet* hizo *criteria* ambazo zimetolewa hapa tatizo lake litakuwa limekwisha. Lakini iwapo halitakuwa lime-*meet* hivyo vigezo tatizo lake litakuwa limebakia pale pale.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali imeshatenga fedha kununua magari kwa ajili ya vituo vya afya ambavyo vina matatizo makubwa. Matatizo ya jimbo la Busanda hayatofautiana sana na matatizo yaliyoko Babati, na jimbo la Busanda lina vituo viwili ambavyo viko mbali sana na wilayani Geita.

Je, katika mpango huo sasa Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia, sasa atavifikiria angalau vituo viwili katika jimbo la Busanda kituo cha Butundwe na kituo cha Bukoli viweze kupata magari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba vigezo nilishavieleza katika swali langu la msingi, iwapo vituo vya afya hivyo ambavyo amevielezea Mheshimiwa Mbunge, vitakuwa na vigezo kama nilivyovieleza katika jibu langu la msingi tatizo lake litatatuliwa. Vigezo hivyo vitaangaliwa kwa undani sana. Kuna vya hospitali na vituo vya afya ambavyo kwa kweli viko mbali sana na hospitali za wilaya, naweza nikatoa mfano mmoja wa Kituo cha Afya kimoja ambacho kipo karibu na Msumbiji, hiki ni kituo cha afya.

Sasa huwezi ukatoa gari kwa hospitali ambazo ziko barabarani au Vituo vya Afya ambavyo viko barabarani ukaacha Vituo vya Afya ambavyo viko mbali kama vile vilivyoko karibu na Msumbiji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mambo haya yamejibiwa vizuri tu. Kwa hiyo, swali linalofuata ni la Mheshimiwa Kwaangw'.

**Na. 18**

**Madai ya Walimu**

**MHE. OMAR S. KWANGW'** aliuliza: -

Kwa kuwa, katika Bunge la Bajeti la 2004/2005 malalamiko ya walimu kutolipwa stahili zao mbalimbali yalijadiliwa kwa kina na hatimaye Serikali kulazimika kuunda TUME:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani ambazo walimu wa shule za msingi, sekondari na vyuo wanadai Serikali kufikia Oktoba, 2005 na Serikali imewalipa kiasi gani hadi kufikia Februari, 2006.

(b) Je, ni asilimia ngapi sasa Serikali imefikia katika kulipa madai ya walimu ambayo yamehakikiwa na inatazamia kumaliza madeni hayo lini?

(c) Je, ni kiasi gani cha madai mapya ya walimu yamelimbikizwa hadi sasa baada ya TUME ya Waziri Mkuu ya 2004 kukabidhi ripoti yake Oktoba, 2004.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kwaangw'; Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mnamo mwezi Agosti 2004 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Tume iliyoongozwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw'; Mbunge wa Babati Mjini, kwa ajili ya kuchunguza madai mbalimbali ya walimu vile vile Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mwezi Juni 2004 ilikuwa imeunda Tume ya uhakiki wa madai ya walimu na watumishi wengine wa Halmashauri. Tume hii iliundwa na Wajumbe kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na pamoja na Halmashauri zenyewe.

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya uhakiki wa Tume hiyo, baadhi ya madai yalikataliwa kutokana na kutokidhi taratibu na kanuni za ulipaji wa fedha za Serikali. Madai yaliyokubaliwa yaliwasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo. Kulingana na taarifa zetu mpaka hivi sasa madai yaliyo hakikiwa ya walimu wa shule zamsingi ni shilingi bilioni 2.8. hadi kufikia Februari, 2006 Serikali iliwalipa walimu jumla ya Shilingi billion 2.6. Aidha, Serikali inadaiwa jumla ya Sh.200,551,796.10 hadi Oktoba, 2005.

(b) Mheshimiwa Spika, malipo ya madai ya walimu ambayo yamekamilika na kulipwa ni asilimia 98.4. madai yaliyohakikiwa na hayajalipwa na yale ambayo wadai wake hawakujitokeza, ndio hayo madai ambayo yanadaiwa Serikalini. Hivyo, madai hayo yatalipwa mara tu wadai watapojitokeza kwa sababu fedha hizi zipo.

(c) Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wameelekezwa kutolimbikiza madeni yoyote tena ya watumishi wakiwemo walimu baada ya Serikali

kuongeza viwango vya ruzuku inayotolewa kwa wahusika. Hivyo, kwa uratibu huo hakuna tena malimbikizo ya malipo ya madai ya walimu katika shule za msingi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri hakujibu madai ya walimu wa Sekondari na Vyuo kama ilivyo kwenye swali 18 kipengele (a) yametolewa tu majibu ya madai ya shule za msingi. Sasa ningependa kufahamu sekondari na vyuo kama ilivyoainishwa kwenye swali.

(ii) Kwa kuwa, hii tabia ya walimu kuvumilia kwa muda mrefu ilijengwa na Rais wa Chama cha Walimu Tanzania Mheshimiwa Margreth Sitta na kwa kuwa sasa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania ndiye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na ndio mwenye dhamana ya kuimarisha elimu na vilevile kulinda maslahi ya walimu. Je, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anawapa walimu matumaini gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumjibu Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo;

Ni vizuri kabisa kukiri hapa kwamba nilishajiuzulu nafasi ya Urais wa Chama cha Walimu, halafu pia nilishajiuzulu Uenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi TUKUTA kutokana na mimi kuteuliwa kwa nafasi niliyo nayo. Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa sababu inanipa nafasi ya kushughulikia matatizo ninayoyafahamu ya walimu na sekta nzima ya elimu, kadri ya uwezo wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuhusu madai ya walimu, mimi ningeomba tusubiri kwa sababu liko swali namba 28 la leo ambalo litajiwa na Naibu Waziri kama lilivyoandaliwa. Lakini ama sivyo niko tayari kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI kushughulikia madai ya walimu kwa sababu mimi nasimamia utekelezaji wa sera za elimu. Kwa hiyo, ni lazima pia nishirikiane naye katika kuangalia namna ambavyo inatekelezwa kwa kuangalia pia maslahi ya watekelezaji. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, katika kipindi kisichopungua miaka mitatu sasa Bajeti ya Serikali imekuwa haina naksi na kwa kuwa malipo ya mishahara yote yanatoka kwenye mfuko mkuu wa Serikali wa Hazina;

Je, Serikali inaweza kueleza ni sababu zipi zinaendelea kuwakopa watumishi kwa mfano jeshi la polisi linadai bilioni 8.5 hivi sasa kuna sababu yoyote ya msingi wakati fedha zote zinatoka kwenye mfuko wa Serikali na bajeti haina naksi?

**SPIKA:** Naona hili swali linaleta hoja mpya kabisa ambayo haiambatani na swali la msingi, kwa hiyo tunaendelea. (*Makofi*)

**Na. 19**

**Ikulu ya Wete Pemba**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza: -

Kwa kuwa Kisini Pemba kuna Ikulu ya Wete ambayo ni Ikulu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa, Ikulu hiyo haina hadhi inayotakiwa kwani majengo yake yamechakaa mno, fenicha mbovu na barabara zinazoingia hapo ni mbaya sana; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya tatu aliahidi kukarabati Ikulu hii: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Ikulu hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa Mheshimiwa Rais atashindwa kupumzika eneo hilo wakati wa ziara zake sehemu hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Ikulu ndogo ya Wete inamilikiwa na kuendeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo, jukumu la kuikarabati na kuihudumia Ikulu hiyo liko mikononi mwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba iwapo Mheshimiwa Rais atakwenda Pemba kwa ziara itakuwa ni vigumu kufikia hapo kwa sasa kwa sababu ya hali mbaya ya Ikulu hiyo. Ofisi yangu itapeleka suala hili rasmi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili waweze kuikarabati Ikulu hii kama inavyotakiwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa sambamba na ubovu wa Ikulu ya Wete, lakini pia kuna ubovu zaidi wa Ikulu ndogo ya Chake Chake ambayo ndiyo wanayofikia Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, Ikulu hiyo pia itatengenezwa lini maana yake haikaliki kwa hafikii hapo siku hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba inategemeana

umiliki wa Ikulu hizi uko mikononi mwa Serikali ipi, endapo Ikulu hii ya Chake Chake kama ilivyo ile ya Wete itakuwa chini ya mikononi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tutafanya mawasiliano ili waweze kuzikarabati Ikulu zote mbili. Lakini endapo kama ilivyo kawaida ya Serikali mbili hizi kusaidiana ninakumbuka vilevile kwamba kipindi cha nyuma Serikali ya Muungano ilitoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu ile ya Wete. Ni utamaduni wetu wa kusaidiana kati ya Serikali zetu mbili bila shaka hilo tutalifuatilia na endapo itaonekana kwamba fedha hiyo inaweza kupatikana basi ukarabati utafanyika kutoka Serikali ya Muungano.

**Na. 20**

**Vijiji Visivyopimwa**

**MHE. ZITTO K. ZUBEIR** aliuliza: -

Kwa kuwa vijiji vitano (5) tu kati ya 33 vya Jimbo la Kigoma Kaskazini vimepimwa: -

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni hatari kuwa na ardhi ya vijiji ambavyo havijapimwa?

(b) Je, kwa nini vijiji vya Kigoma Kaskazini havijapimwa? na

(c) Kwa kuzingatia mpango wa MKURABITA, Serikali haioni kuwa ni busara sasa ardhi ya Jimbo la Kigoma Kaskazini ikapimwa ili wananchi waendelee kumiliki ardhi kihalali?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zubeir; Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria za Ardhi, zinaelekeza kuhusu upimaji wa ardhi nchini kote. Pia, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 aya ya 42, kifungu (b), kinaelekeza kuwa Serikali itahakikisha kuwa hatua zinachukuliwa za kuendeleza kwa nguvu mpya kazi inayofanywa na Halmashauri za Wilaya katika kutambua mipaka ya wilaya, mipaka ya vijiji, kupima na kuvipatia vijiji vyeti vya ardhi, ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini.

Hivyo, Serikali inafahamu kuwa bila ya ardhi ya kijiji kupimwa itakuwa hatarini kugawiwa kwa watumiaji wengine bila ya Mamlaka husika kujua. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi na kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji iliyobaki nchini ili kuondoa hatari zinazotokana na vijiji kutokupimwa.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya vijiji 34 kati ya vijiji vipatavyo 240 vimepimwa katika Mkoa wa Kigoma, vikiwemo vijiji vitano katika Jimbo la Kigoma Kaskazini.

Pia, kuna jumla ya vijiji 34 vingine ambavyo vimefanyiwa upimaji wa awali katika mkoa huo na kazi ya kukamilisha upimaji inaendelea. Vijiji vingi havijapimwa katika Mkoa huo kutokana na uwezo mdogo wa Serikali wa kugharamia kazi hiyo. Gharama ya upimaji wa kijiji kimoja inakisiwa kuwa ni Shilingi 1,500,000.

Halmashauri za Miji na Wilaya kwa kushirikiana na wananchi, zinatakiwa kuchangia gharama ili kuongeza kasi ya upimaji. Aidha, Serikali imeandaa Mpango wa Kimkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi (*Strategic Plan for Implementation of Land Laws* (*PILL*) kwa kushirikiana na wafadhili ikiwemo Benki ya Dunia (*World Bank)* kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango wa MKURABITA ni muhimu vijiji yote vikapimwa. Serikali imekwishaanza kutekeleza mpango huo wa kurasimisha raslimali ardhi kwa lengo la kuwanufaisha Watanzania walio wengi. Hata hivyo, tatizo la fedha ndilo linakwamisha. Serikali itaendelea kugharamia upimaji huo kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana lakini nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa, baadhi ya vijiji vya Jimbo la Kigoma Kaskazini vinapakana na Hifadhi ya Gombe na kuna mipango ya kupanua Hifadhi ya Gombe, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ni muhimu sasa vijiji hivi vikapewa kipaumbele kupimwa ili wapate vyeti mapema vya kumiliki ardhi ili baadaye vijiji visije vikachukuliwa kama sehemu ya Hifadhi ya Gombe?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto, kama ifuatavyo:-

Katika nchi nzima tuna Vijiji 12,000, tumekwishapima Vijiji 6,000 na tuna mpango wa kupima Vijiji 1,500 kila mwaka, tutazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kufuatana na upatikanaji wa fedha na kuhakikisha kwamba kijiji hicho kinapimwa ili kuwezesha kisije kikachukuliwa kwa manufaa mengine.

**Na. 21**

**Mradi wa *Finland Water Profect – MPARA***

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mradi wa Maji wa *Finland Water Project* uliofadhiliwa na kutekelezwa kwa asilimia 80 na Serikali ya Finland kwa miaka ishirini iliyopita umeachwa bila kukamilika; na kwa kuwa, wananchi wa Mpara – Kilwa Masoko waliutegemea sana mradi huo, lakini kutokana na kutekelezwa kwake, mashine na vifaa mbalimbali vya mradi vimechakaa sana na vingine vimeibiwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuufufua mradi huo na kukamilisha asilimia 20 iliyokuwa imebaki ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji?

(b) Je, Serikali inaweza sasa kulieleza Bunge hili kwamba ni lini hasa kazi ya kuufufua mradi itaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kwanza kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini , nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa maji Kilwa Masoko ulianza kujengwa mwaka 1980 kwa ajili ya wakazi wa Kilwa Masoko na pia kwa ajili ya Kiwanda cha Mbolea kilichotegemewa kujengwa katika eneo hilo. Mkandarasi wa mradi huo ilikuwa ni kampuni ya *FINWATER* kutoka Finland. Ujenzi wa mradi ulisimama mwaka 1995 kutokana na Serikali ya Finland kusimamisha utoaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kilwa Masoko una wakazi 13,374 ambao wana mahitaji ya lita 1,500,000 za maji kwa siku. Vyanzo vya maji vipo katika kijiji cha Mpara. Gharama ya kukamilisha mradi huo kwa sasa inakadiriwa kuwa shillingi 211,176,885/=

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina mpango wa kufufua na kukamilisha mradi huo. Pia katika mwaka 2004/2005 Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuchimba visima 2 ambapo kimoja kilikuwa kwenye sehemu ya mikoroshini na kingine katika sehemu inayoitwa Bustani ya Mkapa.

Visima hivyo vilichimbwa na maji yamepatikana, kwa pamoja visima hivyo vinatoa lita 52,000 kwa saa. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2005/2006 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 130,000. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi huu.

(b) Kama nilivyoeleza kwenye kipengele (a), Serikali ilianza kutenga fedha kuanzia mwaka 2004/2005 kwa ajili ya kuchimba visima vingine viwili ambavyo vitaongeza upatikanaji wa maji na kujenga tanki la kuhifadhi maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumeahidi kwama tutaendelea kutoa fedha mwaka hadi mwaka kwa ajili ya mradi huo tukizingatia kwamba bajeti yetu ni finyu lakini pia kero ya maji ni kubwa nchi nzima kwa hiyo bajeti ndogo tutagawa kila upande angalau mwaka kwa mwaka tutimize miradi hiyo. (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE**:- Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, mradi huu wa *FINWATER* ulikuwa unahudumia mikoa yote ya Lindi na Mtwara na uliisha ghafla kama hivyo alivyozungumza Naibu Waziri.

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuwa na mpango mbadala wa kuhudumia hasa maji vijijini na katika hili nataka kusema katika Jimbo la Masasi kwa sababu hali iko mbaya kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama jinsi nilivyosema awali kwamba Serikali itajitahidi kutenga fedha lakini hata hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali pia ina miradi ya maji katika Wilaya ya Masasi na ningependa nimfahamishe miradi gani ambayo sasa hivi Wilaya ya Masasi inashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Masasi ina miradi kumi ya maji ifuatayo katika Vijiji nitakavyovitaja:-

Katika kijiji cha Chikoweti, Mlingula, Nanganga, Nanyumbu, Mpeta, Namkwingu, Kilosa, Chiwale, Namasogo na Kijiji cha Msanga.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Sambamba na huu mradi wa Finland unaofadhiliwa huko Kilwa Kusini vilevile Musoma Mjini tunao mradi unaofadhiliwa na Wafaransa, lakini mradi huu umeanza toka mwaka 2002 hadi sasa hakuna ambacho kimeshaendelea pamoja na kwamba Musoma Mjini iko jirani sana na maji kwa maana ya Ziwa Victoria. Je, Labda Naibu Waziri anisaidie kwamba Serikali ina mpango gani wa kuweza kuingilia suala hili kati ili msukumo uweze kuwepo na watu wa Musoma waweze kupata maji mbali na tabu wanayoipata ambayo sasa ni ya muda mrefu?Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ukipenda unaweza kulijibu lakini ukipenda pia linaweza likachukua sura ya swali jipya baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Naomba liwe swali jipya.

**SPIKA:** Unaomba ujibu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Hapana hili ni swali jipya.

**SPIKA:** Liwe swali jipya. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Ah**!** Mheshimiwa Mbona umeketi tena umekata tamaa, kwa kuwa hili limekuwa batili basi nakupa nafasi uulize

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako mazuri kuhusu huu mradi wa maji wa Kilwa lakini bado hapa kuna utata kwa majibu uliyoyajibu yanaelezea maji katika Makao Makuu ya Wilaya na siyo Kijiji cha Mpara ambako ndiyo chimbuko la maji yenyewe. Wao bomba la maji linapita pale na chanzo cha maji kiko pale lakini wao hawana maji lakini huu mradi ulikuwa umelenga pale.

Kwa hiyo, mimi ninachooliza ni je, wawe na matumaini lini ya kupata hayo maji kwa kuwa wana shida sana ya maji?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nimemuelewa Mheshimiwa Mbunge swali lake anauliza kwamba Vijiji hivyo vya hapo vitapata maji lini kwa sababu haya maji yanakwenda Mjini Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba katika kijiji cha Mpara kimechimbwa visima, ambacho pia na vyenyewe vinaongezwa na katika jibu langu B nimesema kwamba kuna visima vingine viwili vitaongezwa na hivyo ni katika kijiji cha Mpara. (*Makofi*)

Na. 22

**Upatikanaji wa Maji Kinondoni**

**MHE. IDD M. AZZAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, ukame, uchakavu wa mabomba na mitambo ya kusukuma maji vimeathiri kwa kiwango kikubwa upatijanaji wa maji katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Kinondoni hasa Kigogo, Magomeni, Mwananyamala, Kinondoni, Ndugumbi na Tandale; na kwa kuwa, kutokana na hali hiyo, wananchi wa maeneo hayo hutumia maji yasiyo

salama, hivyo kusababisha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu ambacho kinasababisha vifo vingi vya watu:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuchimba visima virefu kwenye maeneo hayo kuasaidia wananchi upatikanaji wa maji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuwahakikishia wananchi wa maeneo hayo kwamba, watapata huduma bora ya maji safi ya bomba majumbani mwao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, swali lake lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ukame, uchakavu wa mabomba na mitambo ya maji imeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na maeneo ya Jimbo la Kinondoni. Serikali kuptia Shirika la Maji *DAWASA* inatekeleza Mradi wa uboreshaji huduma ya Majisafi na Majitaka kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 164.6, kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambao wanatoa dola za Kimarekani milioni 65.55, Benki ya Maendeleo ya Afrika wanatoa dola za Kimarekani milioni 48, Benki ya Raslimali ya Nchi za Ulaya wanatoa dola za Kimarekani milioni 35, *DAWASA* yenyewe inatoa dola za Kimarekani milioni 14.05 na *DAWASCO* inatoa dola za Kimarekani milioni 2. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2003 na utakamilika mwaka 2007. Mradi huu utahusu ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka na pia programu ya Miradi ya Kijamii ya Maji na Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, chini ya programu ya Miradi ya Kijamii ya Maji na Usafi wa Mazingira (*Community Water Supply and Sanitation Program*), baadhi ya maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yamepangwa kuchimbiwa visima virefu. Aidha, chini ya mpango huo, maeneo ambayo hayafai kuchimba visima virefu yatawekewa magati ambayo tunasema (*Water Kiosks*) ambapo wananchi watakuwa wanachotea maji sehemu hizo. Kazi hizi zinatekelezwa kwa kushirikisha wananchi na kukaratibiwa na Asasi isiyo ya Kiserikali ya *Plan International*. Tayari utekelezaji umeanza katika maeneo ya Mwananyamala Kisiwani ambako kisima imechimbwa na maji yamepatikana. Pia awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa magati ulianza Januari, 2006 na maeneo yatakayofaidika na miradi hii ya kijamii ni katika Jimbo la Kinondoni ni Magomeni, Ndugumbi, Tandale, Kinondoni, Mwananyamala, Makumbusho, Sinza na Hananasif.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU**: Mheshimia Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia imani, lakini bado kuna uhaba wa upatikanaji maji wenyewe kutoka Mto Ruvu.

Mheshimiwa Spika, jimbo la Ilala linakumbwa sasa hivi na maradhi ya kipindupinddu kutokana na maji kutokuwa salama. Je, mipango yote mizuri ya Serikali inafanya

miundombinu hii inayoitoa sasa hivi kuwa na mpango wowote wa Serikali kuvuta maji kutoka Mto Rufiji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zungu, Mbunge wa Ilala. kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika ni kweli kabisa kwamba maji ya Dar es Salaam yana uchakavu na pia kwa kufuatana na sababu ambazo nimesema awali ni kwamba tunajitahidi kushughulikia lakini hata hivyo mto Ruvu una sababu nyingi ambazo imefanya kwamba maji yake yasiweze kutosheleza na hatimaye kuwa machafu.

Sababu zikiwemo kwamba tatizo moja kwa mto wa Ruvu ni kwanza pampu haitoshelezi lakini kwa wakati huohuo maji machache yanayokwenda Dar es Salaam njiani watu wanayakata na katika kukatika mabomba huko njiani uchafu wa aina mbalimbali pia unaingia kwa bahati mbaya lakini kitu ambacho mimi ningeweza kushauri ni kwamba Mheshimiwa Mbunge atusaidie katika kuelimisha wananchi wachemshe maji wasiyaamini jinsi yalivyo.

Pili Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba je, chanzo cha Rufiji kwa nini kisitumike. Katika mikakati ya Wizara yangu Rufiji pia ni mojawapo ambayo imo katika kufikiria na pia kuifanyia upembuzi yakinifu ili maji hayo pia tuone uwezekano wake lake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama nilivyosema awali Bajeti yetu ni finyu jambo hilo siyo la haraka na siyo la kwamba la hivi sasa ni jambo ambalo litakuwa ni la muda mrefu lakini limo katika programu yetu na ninamuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ikiwa upembuzi yakinifu utafaa basi kitu hizo pia kitashughulikiwa hapo baadaye. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ili kumalizia Wilaya ya Dar es Salaam, Mheshimiwa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri, lakini mimi ombi langu ni moja mimi nimeelewa nilikuwa namwomba tu Mheshimiwa Naibu Waziri aeleze ili na wananchi wa Temeke waelewe kwamba wako kwenye mpango huu awatamkie tu kwamba Temeke na ninyi mpo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Temeke nalo pia hatukulisahau katika mambo ya maji, napenda kumtajia sehemu ambayo mradi huu utanufaisha Jimbo lake la Temeke na Wilaya nzima ya Temeke.

Sehemu zitakazonufaika ni Temeke yenyewe pale, Chang'ombe, Keko, Miburani, Kurasini, Mtoni na pia Mbagala. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali Namba 23 majibu yake hayajawa tayari kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Captain Mkuchika karibu. *(Makofi)*

Na. 24

**Viwanda vya Kubangua Korosho**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Kwanza ilijenga viwanda kumi na moja hapa nchini kwa ajili ya kubangua korosho na kuuza nje ya nchi pamoja na kutoa ajira kwa wananchi.

(a) Katika ubinafsishaji wa viwanda hivyo, Je, ni viwanda vipi vimeuzwa, vingapi vimekodishwa na vingapi wawekezaji wameingia ubia na Wantanzania?

(b) Kati ya viwanda hivyo, ni viwanda vingapi vinafanya kazi na vimeajiri watu wangapi?

(c) Je, ni hatua gani iliyofikiwa katika ubinafsishaji wa viwanda vya Newala A na Newala B

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji napenda kumjibu Mheshimiwa Captain George Mkuchika, Mbunge wa Newala, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, viwanda 8 kati ya 12 vilivyopo vimeuzwa kwa Watanzania kwa asilimia 100 navyo ni:-

(i) *Kibaha Cashew nut processing factory;*
(ii) *Mtwara Cashew nut processing factory;*
(iii) *Likombe Cashew nut processing factory;*
(iv) *Masasi Cashew nut processing factory;*
(v) *Newala I Cashew nut processing factory;*
(vi) *Newala II Cashew nut processing factory;*
(vii) *Tanita I Cashew nut processing factory;*
(viii) *Lindi Cashew nut processing factory.*

Viwanda vine (4) vilivyobakia vipo katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji navyo ni:-

(i) *Tunduru Cashew nut processing factory;*
(ii) *Tanita II Cashew nut processing factory;*
(iii) *Mtama Cashew nut processing factory;*
(iv) *Nachingwea Cashew nut processing factory.*

(b) Mheshimiwa Spika, ni kwenda cha Masasi pekee ambacho kinafanya kazi. Ubanguaji ni wa msimu na kwa msimu wa mwaka jana 2005 waliajiri wafanyakazi 550. Kwa upande wa kiwanda cha Tanita I uuzaji wake haukuweka sharti la kuendelea na shughuli za ubanguaji wa korosho. Kwa kuwa kutoweka sharti kulisaidia kuuza kwa bei kubwa ambayo iliweza kukabiliana na madeni ya viwanda vya korosho.

Pia, huduma ya ubanguaji wa korosho za mkoa wa Dar sa Salaam itafanyika katika kiwanda cha Kibaha Mkoa wa Pwani. Viwanda 6 vilivyosalia viko katika hatua ya kukarabatiwa. Wawekezaji wamepewa muda wa miaka 2 kuanzia mwaka jana (2005) kulingana na tarehe waliozokabidhiwa viwanda. Makabidhiano yalifanyika kama ifuatavyo:-

(c) Mheshimiwa Spika, kiwanda cha Newala I kimeuzwa kwa kampuni iitwayo *AGROFOCUS*, na kipo katika maandalizi ya ukarabati. Kiwanda cha Newala II kimeuzwa kwa kampuni iitwayo *MICRONIX*, nacho kipo katika hatua ya kukarabatiwa.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kila mradi unaobinafsishwa yule anayoomba kupewa anawasilisha Serikalini *investment plan* ambayo inaelezea anaonyesha *programme* yake ukarabati utachukua muda gani, kiwanda kinategemewa kuanza lini na kadhalika, tulivyosikia nilidhani ni Newala tu karibu viwanda vyote vilivyobinafsishwa hakuna kinachofanyika.

Je, kuhusu Newala Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa *Newala Investment Plan* iliyowasilishwa katika kubinafsisha Newala I na Newala II lini walisema viwanda hivyo vitaanda kukarabatiwa na kufanya kazi kwa sababu mpaka sasa hivi hakuna chochote kilichofanyika na hata wale walinzi wanaolinda pale hawana mshahara. (*Makofi*)

Ni azma ya Serikali ya Nne kuongeza ajira watu milioni moja, Newala I na Newala II ikifanya kazi itaajiri akina mama 4000, baada ya kuona wawekezaji wanasuasua Serikali inawapa matumaini gani wananchi wa Wilaya ya Newala kuhusu kufufuka kwa viwanda vyao yaani Newala I na Newala II. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mkuchika maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kubangulia korosho vilikuwa havifanyi kazi kwa zaidi ya miaka 25 *to an extent* kwamba Wabunge waliopita waliviita viwanda hivyo *White Elephants*.

Ni majuzi tu kuanzia mwaka 2004 na kupitia kwa *pressure* ya Wabunge kumuomba Waziri Mkuu kupunguza masharti yaliyowekwa ya ubinafsishwaji ndiyo viwanda hivi vilianza kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba viwanda hivi vinane ndivyo ambavyo vimeshabinafsishwa na vimebinafsishwa kwa Watanzania mia kwa mia lakini viwanda vinne viko katika hatua mbalimbali ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, Newala I na Newala II kama ambavyo tumesema vimepata wawekezaji wawili *MICRONIX* pamoja na *AGROFOCUS*. Wawekezaji hawa wamepewa miaka miwili kuanza kukarabati viwanda hivi na kwa kweli hawa wawili niliowataja wameshaanza na wako katika hatua mbalimbali za ukarabati.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali na hususani awamu ya nne kukazia sana suala la ajira na ni katika azma hii basi ndiyo maana Serikali imetoa miaka miwili ya viwanda hivyo kuanza kuonyesha kwamba wanafanya kazi ili waweze kuajiri na hivyo kuongeza ajira na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Samahani majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kutoa maelezo ya nyongeza kama ifuatavyo:

Nayo ni kwamba mimi na mwenzangu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tumo katika ushauriano hatua za mwisho za ushauriano juu ya kuweka utaratibu ambao utawafanya wafanyabiashara na wanunuaji wa korosho kwa kutumia taratibu za kodi waone inafaa kwao kuuza nje korosho zilizobanguliwa kuliko zile korosho ambazo hazijabanguliwa. (*Makofi*)

Nina hakika tukiweka utaratibu huo kwa kutumia njia za kodi tukishirikiana na mwenzetu Waziri wa Fedha tutawezesha zaidi ubanguaji wa korosho ndani ya nchi kwa hiyo *capacity* yote ya viwanda itaweza kutumika kwa njia hiyo. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Mkuchika awe na subira na tushirikiane naye kupeana mawazo zaidi ili tuweze kukamilisha maamuzi haya kupitia Bajeti inayokuja. (*Makofi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika jibu la msingi alisema katika viwanda vinane vilivyobinafsishwa mia kwa mia, kiwanda cha korosho cha Kibaha pia Tanita Kibaha kimebinafsishwa.

Je, atatueleza nani aliyenunua kiwanda hiki na ataanza kazi lini? Na je, wale wafanyakazi ambao hawajalipwa mpaka leo katika yule mwekezaji wa kwanza nani atawalipa?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kiwanda cha kubangulia korosho cha Kibaha kimebinafsishwa mia kwa mia na kwa Watanzania. Mtanzania ambaye ameuziwa kiwanda hiki ni *Sulphur Petroleum Limited.* Lakini tunajua au Serikali inajua kwamba kulikuwa na washindani wengine wawili, mmoja kwa jina la Bwana Omar na mwengine ni Bwana Rashid Malima ambao nao walikuwa wamefanya *competitive bidding* ya viwanda hivi.

Lakini Bwana Omar ambaye ndiye alikuwa amepangishwa na Bodi ya Korosho hapo awali alikuwa mkorofi kidogo kwa sababu alikuwa halipi pango. Kwa hiyo, katika *bidding* hakushinda lakini vilevile kulikuwa na Ndugu Rashid ambaye *bidding* yake ilikuwa ni chini ya matarajio ya *tender.* Kwa hiyo, naye hakupata. Kwa hiyo, aliyepata ni Ndugu *Sulphur Petroleum Limited* na ameshaanza ukarabati wa kiwanda hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi, ndiyo maana tumesema kwamba Tanita I ilibinafsishwa bila masharti na kwa namna hiyo tuliweza kupata fedha za kutosha. Serikali imeweza kupata kiasi cha shilingi bilioni 1.42. Kwa hiyo, fedha za Tanita I zitasaidia kulipa wafanyakazi walioachwa katika kiwanda cha Kibaha. (*Makofi*)

**Na. 25**

**Watumishi wa Idara ya Mifugo**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imegawa Wizara ya Maji na Mifugo kuwa Wizara mbili tofauti na kwa kuwa, kwa miaka iliyopita Idara ya Mifugo ilikuwa Wizara ya Kilimo, na tangu wakati huo watumishi wa Wizara hizo wamekuwa hawatoshelezi kwenye Halmashauri zote nchini.

Je, Serikali itaajiri lini watumishi wa kutosha kwenye Idara ya Mifugo ili Halmashauri zipate watumishi wa kutosha na kutoa Elimu bora kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba idadi ya watumishi wa Sekta ya Mifugo katika Halmashauri zetu hawatoshi; kwa mfano kati ya karibu vijiji 10,000 vilivyopo nchini ni asilimia 30 hadi 40 tu ya vijiji hivyo ndivyo vinapata huduma kamilifu, kwa maana ya kuwa na Afisa Mifugo katika kijiji.

Katika baadhi ya vijiji huduma hiyo hutolewa na watumishi wa Sekta ya Kilimo, waliopata mafunzo katika fani za mifugo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wataalam wa aina hiyo wanapatikana, Wizara yangu inasimamia na kuendesha Vyuo sita (6) vya mafunzo ya mifugo nchini.

Vyuo hivyo vinatoa wataalamu wa mifugo ngazi ya Astashahada na Stashahada na pia kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji kutoka sehemu mbalimbali nchini.

Kuanzia mwaka 2000/2001 mpaka 2004/2005 Vyuo hivyo vimetoa jumla ya wahitimu 1491, ambao ama wameajiriwa na Halmashauri za Wilaya au Sekta binafsi na baadhi yao ni waajiriwa waliokuwa wanajiendeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002, Halmashauri za Wilaya na Miji zimepewa mamlaka ya kuajiri watumishi wanaowahitaji, kutenga Ikama na Bajeti baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Hivyo Halmashauri zitaendelea kuajiri watumishi ikiwa ni pamoja na wa Idara ya Mifugo kulingana na hali ya bajeti ya Serikali itakavyoruhusu mwaka hadi mwaka.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa watumishi walioko katika maeneo yetu ni watumishi wanaopima nyama tu Mijini. Lakini Madaktari wapima nyama vijijini hata kwenye Kata hawapo. Je, isingefaa kwamba hawa madaktari wanaopima mifugo katika Kata waongezwe ili mifugo hiyo iweze kupata madaktari wa kutosha au wafugaji waweze kupata washauri wa kuwaelimisha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi Serikali inafahamu kwamba wataalam bado hawatoshi, lakini ina azma ya kuongeza watalaam hao mwaka hadi mwaka. Na kusema kweli mpaka tufike kwenye kiwango ambacho kila kijiji kinakuwa na wataalam si wa

kupima nyama tu, lakini pia wa kushughulikia masuala ya mifugo yote kwa ujumla. Kwa hiyo, Serikali kama nilivyosema itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kupata wataalam ili tuweze kujitosheleza.

**Na. 26**

**Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa nchi mbalimbali duniani zinakabiliwa na janga la Ugonjwa hatari wa Mafua Makali ya Ndege – *Highly Pathogenic Avian Influenza (HPAT) - H5N1,* ambao pia unaambukiza binadamu; na kwa kuwa, ugonjwa huo umesambaa duniani kwa kasi kubwa na kwamba sasa umethibitishwa kuwa umegundulika nchini Nigeria:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za tahadhari za kuhakikisha kuwa ugonjwa huo hatari hauingii hapa nchini?

(b) Je, Serikali imefanya maandalizi gani kuhakikisha kwamba madawa ya kutosha yanakuwepo kukabiliana na ugonjwa huo iwapo nchi yetu itakumbwa na janga la ugonjwa huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege, unaosababishwa na virusi aina ya *H5N1,* unaendelea kuenea kwa kasi sana duniani na hadi sasa mpaka wakati tunakamilisha ripoti hii kulikuwa na nchi 38 zilizogundulika kuwa na ugonjwa huo, lakini mpaka jana jioni ni nchi 46 ndizo zenye ugonjwa huo kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)* nchi hizi zinajumuisha Nigeria, Misri, Niger na Cameroon, kwa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo za tahadhari kuhusiana na ugonjwa huu:-

(i) Kupiga marufuku uingizaji wa ndege pori, kuku na mazao yake kutoka nchi zilizoathirika.

(ii) Kufuatilia ugonjwa huu kwenye njia kuu za mapitio ya ndege pori wahamaji nchini kwa kuchukua sampuli na kuzifanyia uchunguzi kwenye maabara. Kazi hii inafanyika kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Marekani *USAID*, Shirika la Kiufundi la Ujerumani *GTZ*, Chuo Kikuu cha Minnesota cha Marekani, ambao kwa pamoja wamechangia dola za Kimarekani 143,000 na Serikali yetu imechangia shilingi

milioni 100. Hadi sasa sampuli 1142 za ndege pori na 210 wa ndege za kienyeji zimechukuliwa na kupimwa. Kwa bahati nzuri, mpaka sasa sampuli zote hazikuonyesha kuwapo kwa ugonjwa huo.

(iii) Kuna Kamati ya Kitaifa (*Multi-sectoral Nation Task Force*) imeundwa ambayo inashirikisha Wizara za Maendeleo ya Mifugo, Maliasili na Utalii, Afya na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ndiyo mratibu, Mambo ya Ndani na Usalama wa Raia. Aidha, Wadau wa Sekta binafsi pia wameshirikishwa. Kazi ya Kamati hii ni kuishauri Serikali namna ya kukabiliana na tishio la ugonjwa huu.

(iv) Wananchi wamehamasishwa pia na kutahadharishwa kuhusu ugonjwa huu kupitia vyombo vya habari kama magazeti, *radio* na televisheni. Aidha vipeperushi 4,500 na mabango 400 vimesambazwa katika Wilaya zote nchini kupitia vituo vya uchunguzi wa maradhi ya mifugo.

(v) Mikoa na Wilaya zilizoko katika mapitio ya ndege pori wahamaji na maeneo wanayotua ndege hao zimeshauriwa kuunda Kamati za ufuatiliaji wa ugonjwa na kudhibiti uingizaji/utoaji wa ndege, kuku na mazao yake na kutoa elimu kwa wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege hauna tiba. Hata hivyo, Serikali imekamilisha mpango wa tahadhari *(National Avian Influenza: Emergency Preparedness and Response Strategic Plan 2006/2007 – 2008/2009)* wa kukabiliana na tishio la ugonjwa huo. Mpango Mkakati huu unahitaji fedha kiasi cha shilingi milioni 800 kwa dharura kwa mwaka wa kwanza ambazo tunatarajia zitatolewa na Serikali yetu.

Pia Serikali imewasiliana na wahisani mbalimbali wakiwemo Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Marekani, *USAID* na Shirika la Kiufundi la Ujerumani *GTZ* ili kuweza kusaidia katika kutekeleza mpango huu. Mpango mkakati huu ni sehemu ya mkakati mzima wa dunia uliokubalika katika mkutano wa Beijing, China, uliofanyika mwezi wa Januari, 2006 ambapo Tanzania ilishiriki. Kwenye mkutano huo wahisani waliahidi dola za Kimarekani bilioni 1.9. Fedha hizo zitapatikana kupitia mikopo, ufadhili na misaada ya kibinadamu.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu nzuri la Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, ugonjwa huu una dalili gani kwa ndege na binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ugonjwa huu una athari kubwa sana kwa ndege na binadamu. Athari ya mwisho kabisa ni kifo. Ndege au kuku akiathirika hatimaye wanakufa na binadamu wakiugua na wasipate kinga ya kuwazuia dhidi ya maradhi yatokanayo na kupungukiwa na nguvu za

kujikinga dhidi ya magonjwa hayo hatimaye hufa. Kwa hiyo, ni ugonjwa ambao ni hatari kwa sababu hauna tiba. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ugonjwa wa mafua ya ndege tayari umeishaingia Afrika. Je, Serikali ina mpango gani na kunguru wanaozagaa Dar es Salaam na Zanzibar kwani wanaweza kuwa kichocheo kikubwa cha kuambukiza ugonjwa huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa mafua ya ndege unaathiri hasa kuku, bata na ndege wa majini. Kunguru wa India hawajawahi mpaka sasa kupatikana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kuwa tunaelewa tabia ya kunguru hawa ni vizuri wananchi wachukue tahadhari ya kusafisha maeneo yao ili kusudi kunguru hawa wasiweze kubeba uchafu kutoka sehemu nyingine ambao unaweza kuwa na virusi hivi iwapo ugonjwa huu utaingia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuchukue tahadhari dhidi ya kunguru wa India wanaoweza kuwa ndiyo ni chanzo.

**Na. 27**

**Kuongezeka kwa Idadi ya Watoto Yatima**

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA (k.n.y Mhe DR. LUCY S. NKYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya watoto yatima inazidi kuongezeka; na kwa kuwa, kuna idadi kubwa ya vikundi vya watu binafsi wanaowakusanya hao watoto kwenye vituo maalumu kwa nia ya kuwasaidia:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu huo mkusanyiko wa watoto hao yatima katika makazi yasiyokuwa na malezi ya kifamilia?

(b) Je, Serikali inatambua athari za mfumuko wa vituo vya watoto yatima ambavyo havina vyanzo endelevu vya mapato?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha jamii ili iweze kuwahudumia watoto hao katika mazingira ya kifamilia?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwepo kwa mkusanyiko wa watoto yatima katika baadhi ya makazi yasiyokuwa na malezi ya familia. Kuwepo kwa watoto hawa katika vituo hivi ni hatua ya mwisho, kwani lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wanalelewa katika misingi ya kijamii *(Community Based Care*)

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua athari za mfumuko wa vituo vya watoto yatima ambavyo baadhi yake havina vyanzo endelevu vya mapato. Vituo hivi visivyo na vyanzo endelevu vya mapato hushindwa kuwahudumia ipasavyo watoto yatima mara wafadhili wao wanapositisha misaada, na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa watoto hao na kwa kwa jamii. Kama nilivyotangulia kueleza kwenye sehemu A ya swali, suala la watoto yatima kutunzwa katika vituo hivyo ni hatua ya muda tu, wakati wakitafutiwa walezi na baada ya njia nyingine zote kushindikana. Hivyo, nasisitiza kuwa watoto hawa ni vyema walelewe katika familia zao isipokuwa pale ambapo familia hizo hazina uwezo kabisa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa watoto kuishi katika mazingira ya kifamilia na kupata malezi yanayostahili. Wizara yangu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa wanawahamasisha wananchi kwa kutumia mbinu shirikishi kubaini uwezo walio nao katika kuondoa vikwazo vinavyowazuia katika kutumia rasilimali zilizopo kujiletea maendeleo na kujikwamua kiuchumi. Uchumi wa jamii ukikua tatizo la familia kushindwa kuwalea watoto yatima litapungua kwani umaskini huongeza makali ya tatizo hili.

Aidha, Maafisa hawa wanasimamia na kuhamasisha jamii kuhusu haki za watoto kama zilivyobainishwa kwenye Sera ya Maendeleo ya Mtoto ambayo imesisitiza umuhimu wa kuwahudumia watoto yatima na wenye mahitaji maalum katika mazingira ya kifamilia ambapo wataweza kupata malezi na mapenzi ya familia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii ina utaratibu wa kuwaruhusu watu wanaopenda kuasili *(adoption)* watoto wasiokuwa na wazazi wote wawili kuwalea na kuishi nao kama familia. Aidha, upo utaratibu unaofanywa na Idara hiyo kwa kushirikiana na vituo vinavyolea watoto kufanya utafiti kutoka kwa watoto wenyewe na jamii ili kuweza kubaini ndugu au walezi wa watoto hawa na hatimaye kuwarejesha kwenye familia zao.

Mheshimiwa Spika, watoto hupenda na kufurahia kuishi ndani ya familia kuliko kwenye vituo. Hivyo, natoa wito kwa jamii kuwa na tabia ya kuvitembelea kila mara vituo hivyo, ili kuwafariji, kuwapatia misaada na kuwachukua kuishi nao angalau kwa muda ili nao wapate upendo wa familia.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya ambaye anafanya kazi kubwa ya kwanza kuwa na kituo cha kulelea watoto yatima. Lakini pia anafanya kazi ya kusambaza misaada kwa watoto yatima ambao wanalelewa katika familia na hilo ndiyo jambo tunaloomba Asasi mbalimbali zifanye kazi za kupeleka misaada kwa zile familia ambazo zimejitolea kulea watoto hawa yatima. *(Makofi)*

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa sasa hivi watoto yatima idadi yao imekuwa kubwa na vituo vya kulelea watoto yatima vimekuwa ni vichache vya Serikali. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watu binafsi ambao wameamua kujitolea kuwasaidia watoto yatima ili waweze kuwalea vizuri hao watoto yatima?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na Asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinaendesha shughuli za kutoa misaada kwa watoto yatima inafanya jitihada kubwa kuhakikisha misaada inawafikia watoto yatima. Wizara yangu ikiwa ni Wizara ambayo imepewa dhamana ya kuratibu *NGO's* hapa nchini imewaita wale wote wenye *NGO's* ili kuhakikisha wanafanya kazi na kupeleka misaada kule ambako inahitajika.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali imeamua kutoa elimu kwa watoto wote nchini, lakini limejitokeza wimbi kubwa la watoto wenye umri wa kwenda shule baadhi yao hawaendi wameenea mitaani kazi yao ni ombaomba hasa katika Jiji la Dar es Salaam na hapa Dodoma wanaleta kero. Je, Serikali ina mpango gani kuhusu suala hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, inaonekana kama unasoma. Kanuni haziruhusu, lazima swali litoke kichwani. Tunaendelea. Mheshimiwa Amina Mpakanjia, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuwa na swali lifuatalo. Kwa kuwa watoto wengi yatima ndiyo wale ambao huwa wanakwenda kuzagaa mitaani ukiachilia mbali ambao tayari wameisha kusanywa katika vituo.

Je, Serikali kupitia Wizara hii inawasaidia vipi wale watoto ambao wako mitaani wanahangaika, hawana wazazi wala hawako katika vituo. Ni juhudi zipi ambazo zinachukuliwa katika kulitatua tatizo hili?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali la msingi, Serikali ikishirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na hasa ikiongozwa na Idara ya Ustawi wa Jamii chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wao wanaendesha misako ya watoto hao mara nyingi na

wanawapeleka vituoni. Tatizo kubwa lililopo ni kwamba watoto hawa mara nyingi huwa hawapendi kukaa kwenye vituo na mara nyingi huwa wanarudi mitaani.

Hata hivyo, jitihada bado zinaendelea kuhakikisha kwamba kule kwenye vituo kuna mazingira mazuri zaidi ambayo watoto hawa wanaweza kukaa. Kwa mfano, kama Dar es Salaam, kuna Kituo kama cha *Dogodogo Centre* ambapo watoto wanawekwa, lakini mara nyingi hata hapo *Dogondogo Centre* pamoja na mazingira kuwa mazuri wanatoroka. *(Makofi)*

**Na. 28**

**Mpango wa MMEM na MMES Mkoa wa Rukwa**

**MHE. ELIATTA NAMDUMPE SWITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia mpango wa MMES na MMEM imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuleta mabadiliko katika Elimu ya Msingi na Sekondari nchini; na kwa kuwa katika Mkoa wa Rukwa pamoja na kutumia vizuri mpango wa MMEM na MMES bado kuna matatizo kadhaa ya kutatuliwa ili kupata mafanikio zaidi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani katika kuongeza kasi ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu?

(b) Je, ni lini walimu wa kutosha watapatikana Mkoa wa Rukwa ili kukidhi upungufu mkubwa uliopo?

(c) Je, ni lini Serikali italipa madeni ya walimu ya uhamisho, matibabu na kuongeza posho kwa walimu wanaofanyakazi katika mazingira magumu kama wale wanaofundisha kando ya Ziwa Tanganyika ambako usafiri ni mgumu sana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kuongeza kasi ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu ni kuendelea kuunga mkono juhudi za wananchi na Halmashauri katika ujenzi kwa kutoa Ruzuku ya Maendeleo kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa shule za msingi na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES).

Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa MMES Serikali ilitoa Sh.112,00,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 16 na sh.72,000,000/= kwa ujenzi wa nyumba 8 za walimu katika shule mpya za sekondari za Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Aidha, kiasi cha Sh.207,000,000/= zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 23 na Sh.42,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 6 katika shule za zamani.

Serikali katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 imepanga kutoa ruzuku ya Maendeleo kupitia MMES kwa ajili ya kujenga jumla ya Madarasa 1637 na nyumba za walimu 1000 nchini kote.

Kila Wilaya itatumiwa fedha za ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu kulingana na fedha zitakavyopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuajiri na kuwapanga walimu kwa uwiano wa mahitaji kadri inavyowezekana kote nchini. Mwaka 2005 walimu 84 walipangwa kufundisha katika shule za sekondari Mkoani Rukwa. Mwezi Februari, 2006 walimu 43 wamepangwa katika Mkoa huo.

Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kuwapanga wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu moja kwa moja baada ya kuhitimu ikiwa ni hatua mojawapo ya kupunguza tatizo la uhaba wa walimu. Kwa sasa tunategemea wahitimu 3500 wa Stashahada watakaohitimu tarehe 30 Mei, 2006. Watakaopangwa watasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa walimu nchini ukiwemo Mkoa wa Rukwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikilipa madeni ya walimu ya Uhamisho, matibabu, likizo na fedha za kujikimu kwa walimu wa ajira mpya (*First Appointment*).

Kwa wale wanaolipwa na Katibu Mkuu wa Wizara yangu, hadi kufikia Januari, 2006 jumla ya walimu 2753 waliwasilisha Wizarani madai yao yanayofikia Sh.1,692,778,642.60. Hata hivyo, walimu 587 walilipwa jumla ya Sh.323,452,882.30.

Hata hivyo, ili kutambua madeni halisi Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeunda Kamati ya kuhakiki madai hayo ili yalipwe. Ni kweli kuwa wapo walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Serikali inaliangalia kwa makini suala hili la walimu wanaofanyakazi katika mazingira hayo. Hii ni pamoja na kubainisha vigezo vya mazingira magumu na viwango vya posho maalum vya kutolewa kwa wahusika.

**MHE. ELIATTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Ninaomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, ni lini walimu hao wa Rukwa baada ya Wizara ikishafanya mikakati watalipwa fedha zao wanazozidai; na ni lini mipango hiyo ya kuwapa posho maalum kwa wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu itatekelezwa?

(b) Kwa kuwa hali ya elimu katika Mkoa wa Rukwa si nzuri na hali ya wana-Rukwa kwa kiuchumi pia si nzuri. Je, Wizara hii ina mpango gani kuzisaidia Halmashauri za Mkoa wa Rukwa kuharakisha ujenzi wa shule na nyumba bora za Walimu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali nilieleza kwamba kwa hivi sasa madai ya watumishi wanayolipwa kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, watalipwa mara baada ya uhakiki kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kusema kwamba Kamati hiyo inafanya kazi kwa ari mpya, kwa nguvu mpya na kwa kasi mpya. *(Makofi)*

Pili, napenda nikiri kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhamasisha na kuweza kutatua matatizo ya walimu. Na kwa kweli mimi binafsi kwa niaba ya Wizara yangu tumeshaanza kutembelea Mikoa ambayo ina mazingira magumu.

Napenda kutoa wito kwamba hayo yote tutakayoyabainisha tutayafanyia kazi kwa kuwa lengo la Serikali ya Awamu ya Nne ni kuhakikisha kwamba walimu hawapati kero zaidi. *(Makofi)*

**Na. 29**

**Vijana Wanaowasaidia Watalii Kupanda Mlima Kilimanjaro**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mlima Kilimanjaro ni kivutio kizuri sana kwa Watalii, na Watalii wengi hufika kupanda mlima huo na kuhudumiwa na vijana waongoza njia na kubeba mizigo yao:-

(a) Je, Serikali inafahamu hali duni ya vijana hao inayotokana na kutolipwa vizuri na Kampuni za Utalii?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka viwango vya mishahara yao na kuhakikisha kwamba inalipwa?

(c) Je, Serikali inafahamu kwamba, hali duni ya vijana hao inalalamikiwa pia na Watalii wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali duni ya Wabeba Mizigo inayotokana na kutolipwa vizuri na Kampuni za Wakala wa Utalii zinazopandisha Watalii katika Mlima Kilimanjaro. Kampuni zinazopandisha wageni kwenye mlima zinaingia mikataba ya muda mfupi inayoongoza misafara ya utalii kutegemea na kipindi cha kupandisha wageni mpaka kushuka. Mkataba huo huwa umekwisha. Wabeba mizigo huchukuliwa na waongoza misafara kwa ajili ya kubeba mizigo ya wageni wanaopanda milima. Malipo ya Wabeba Mizigo hulipwa na wanaoongoza misafara kutegemea fedha atakazokuwa amelipwa mwongoza msafara na Kampuni ya Wakala ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo, Wizara yangu imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha hali za waongoza misafara na wabeba mizigo. Katika vipindi tofauti, Wizara yangu imekuwa ikiongoza au kushiriki katika vikao na wadau mbalimbali vinavyohusisha maslahi ya waongoza misafara ya watalii na wabeba mizigo *(porters)* kama ifuatavyo:-

* Tarehe 4 Machi, 2006 kulikuwa na Kikao cha Uongozi wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro *(KINAPA)* na Chama cha Wakala wa Utalii *(TATO)*.

* Tarehe 18 Machi 2006 kulikuwa na Kikao cha Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)*, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro *(KINAPA)*, Uongozi kwa maana Mwenyekiti na Katibu wa wabeba mizigo na Kiongozi kwa maana Mwenyekiti wa waongoza misafara ya watalii.

* Tarehe 23 Machi, 2006 kulikuwa na Kikao cha Uongozi wa Chama cha Wakala wa Utalii, Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro na Uongozi wa wabeba mizigo

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Vikao hivyo ni kwamba ilikubaliwa kuwa Wakala wa Utalii *(Tour Operators)* wawalipe Wabeba Mizigo na sio kupitia kwa Waongoza Misafara ya Watalii kwa viwango vilivyokubaliwa awali ikiwa na maana mwezi Julai, 2003.

Aidha, Wizara yangu itakuwa na Kikao cha Wadau wote kuangalia jinsi ya kuboresha malipo kwa waongoza misafara *(Tour Guides)* na wabeba mizigo *(porters)* na utaratibu mzuri utakaotumika.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijapata taarifa kutoka kwa Watalii wanaolalamikia hali duni ya wabeba mizigo. Hata hivyo, kuna taarifa kwamba baadhi ya wabeba mizigo hao huwa wanaficha vifaa vyao vya kazi ili watalii wawaonee huruma na kuwapa fedha za ziada *(tips)* ama vifaa vya kupandia milima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali pia kweli yamekwisha. Yapo matangazo.

Waheshimiwa Wabunge wote waliojisajili kuwa wanachama wa *African Parliamentary Against Corruption (APNAC)* na ambao pia watapenda kujiunga na Chama hicho cha hiari, basi wanaombwa kukutana leo tarehe hii ya 29 Machi, 2006 katika Ukumbi Na.231 ghorofa ya pili ya jengo la Utawala saa 7.00 mchana huu.

Pili, Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wameombwa na Mwenyekiti wakutane katika Kikao muhimu sana leo bila kukosa saa 5.00 asubuhi Chumba Na. 227.

Waheshimiwa Wabunge inaelekea kazi za Kamati mbalimbali zilizokabidhiwa Miswada hazijakamilika na kwa mujibu wa Kanuni ya 70 Spika hawezi kuendelea na Miswada hasa kwa hatua ya *Second Reading* kama hajapewa taarifa na Wenyeviti wa Kamati juu ya kukamilisha kazi zao.

Hata hivyo, ninayo matumaini na kwa kweli nawasihi hasa Kamati ya Fedha na Uchumi waweze kukamilisha kazi zilizopo ili tuweze kuingia *Second Reading* saa 11.00 leo kwenye Kikao cha jioni. Nashukuru kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameitisha Kikao nadhani kwenda kuhitimisha kazi hiyo. Nitakuwa Ofisini, nitashukuru kupata taarifa kwamba kazi imekamilika ili saa 11.00 tuweze kuendelea na Miswada.

Kwa hiyo, nitatoa *amended Order Paper* ili kuwezesha wachangiaji wa Miswada tuweze kuingia kwenye *Second Reading* saa 11.00. Ninayo matumaini makubwa na naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi atusaidie ili hayo yaweze kufanyika.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa Katibu aendelee na agenda inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa Mwaka 2006 *(The Bank of Tanzania Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha wa Mwaka 2006**
***(The Banking and Financial Institutions Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria ya Nyama wa Mwaka 2006**
***(The Meat Industry Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria ya Usambazaji wa Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006**
***(The Universal Communications Access Service Bill, 2006)***

*(Miswada Minne iliyotajwa hapo juu ilisomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni)*

*(Saa 04.38 asubuhi Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona, tumekuwa na Nyongeza ya Shughuli za Bunge, nadhani kila mtu anazo pamoja na mabadiliko mbalimbali katika Sheria zitakazotajwa. Kwa hiyo, nadhani kila mtu anayo hiyo nyongeza.

**Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa mwaka 2006**
***(The Bank of Tanzania Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa mwaka 2006, yaani *The Bank of Tanzania Act, 2006* pamoja na marekebisho yake ambayo naamini mmekwishakabidhiwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uwenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Mwinyi Haji Makame, Mwakilishi wa Jimbo la Dimani pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao walishiriki katika kuujadili na kutoa ushauri kuhusu Muswada huu mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi ilipokutana Mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo imesaidia sana kuboresha Muswada huu. Vile vile, nawashukuru sana wadau mbalimbali katika Sekta ya Mabenki ambao wametoa ushauri wao ambao kwa kiwango kikubwa tumeuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba Sheria ya sasa ya Benki Kuu sura ya 197 ya mwaka 1995 ilitungwa takribani miaka kumi iliyopita. Tangu kutungwa kwa sheria hii yametokea mabadiliko makubwa ya kiuchumi kitaifa na duniani kote. Marekebisho yanayopendekezwa kuwasilishwa katika Muswada huu yanalenga kukidhi mabadiliko haya yanayoendelea kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Muswada huu ya kutunga Sheria Mpya ya Benki Kuu tunayoyaleta mbele yenu, yamefanywa ili kwenda sambasamba na mabadiliko mbalimbali ya sera za kiuchumi na kimataifa kwa lengo la kukuza uchumi, kupunguza mfumuko wa bei, kuongeza akiba, kuhakikisha mikopo inapatikana na kadhalika. Ili kufanikisha malengo haya, Serikali inapaswa kusimamia Sera ya Mapato na Matumizi yaani *Fiscal Policy* ambapo Benki Kuu itasimamia sera ya kifedha yaani *Monetary Policy.*

Hivyo basi, Muswada uliopo mbele yenu unakusudia kuweka bayana mgawanyo wa shughuli za kiuchumi baina ya Serikali na Benki Kuu, ambapo Serikali itahusika na Sera za Mapato na Matumizi na Benki Kuu itahusika na Sera za Kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaelezea kwa kirefu maudhui ya Muswada, naomba kutoa maelezo ya maeneo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu kama ifuatavyo:-

Kwanza, Benki Kuu imeongezewa uwezo wa kusimamia Sekta ya Kibenki vizuri zaidi hasa kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Benki na Taasisi za Fedha na pia kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya mawasiliano na ya kibenki.

Pili, pamoja na umuhimu wa kuongeza uhuru wa Benki Kuu katika kutekeleza majukumu yake, Muswada umeainisha umuhimu wa Benki Kuu kuwajibika kwa Serikali na umma kupitia kwa Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Fedha. Vifungu Na. 7 (3), 11 (10), 21 (1) na 21 (3) vya Muswada vinaelekeza Benki Kuu kuwasilisha kwa Waziri wa Fedha taarifa za kihasibu na utendaji kazi wake kwa mwaka. Kuwasilisha *Monetary Policy Statement* katika kipindi cha miezi sita na kuwasilisha taarifa endapo Bodi ya Benki Kuu itashindwa kufikia maamuzi kwa maelewano, yaani *consensus* na kulazimika wajumbe kupiga kura.

Tatu, Muundo wa sasa wa Benki Kuu ya Tanzania utakuwa na Naibu Magavana watatu ambao watateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo katika Muswada huu kifungu cha 8 (3), kinatamka bayana kwamba Rais atateua Naibu Magavana watatu ambao watakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano kama ilivyo kwa Gavana na pia wanaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Aidha, kipindi kifungu hiki kimeweka sharti kwamba katika uteuzi wa Manaibu Gavana hao watatu, mmoja wao atatoka baina ya pande mbili za Muungano. Vile vile, kazi za Manaibu Gavana hao watatu zitaainishwa chini ya Kanuni ndogo ndogo zitakazotolewa na Gavana na kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Ipo katika kufungu cha 13 (10).

Nne, Manaibu Gavana hawa watatu watakuwa na majukumu yafuatayo:-

Naibu Gavana wa Kwanza atahusika na Masuala ya Sera za Kifedha na kuhakikisha uchumi uliotengamaa yaani *Micro-Economy Stability* ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa Sera za Kifedha, masuala ya uendeshaji na usimamizi wa masoko ya fedha, kuandaa Sera zinazohusu mikopo midogo midogo, huduma za kibenki kwa Serikali na utoaji wa sarafu, mahusiano na Taasisi za Fedha za Kimataifa kama vile Shirika la Fedha la Kimataifa *IMF* na Benki ya Dunia, yaani *World Bank*, kuandaa taarifa mbalimbali kwa Serikali kwa ajili ya kuwasilisha Bungeni.

Naibu Gavana wa Pili atahusika na usimamizi wa mabenki ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

Utoaji wa leseni kwa mabenki, Taasisi za Fedha zikiwemo *SACCOS* ambazo mtaji wake umefikia kiwango kilichowekwa kisheria pamoja na kuhakiki menejimenti za mabenki haya, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa mabenki, kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kurekebisha Sekta ya Fedha, yaani *Second Generation of Financial Sector Reform.*

Naibu Gavana wa Tatu, atahusika na usiamamizi wa mfumo wa malipo, utawala, teknolojia ya habari na mawasiliano na uratibu wa masuala ya fedha. Majukumu yake yatajumuisha pamoja na yafuatayo:-

Kusimamia na kuendeleza mfumo wa kisasa wa malipo, maandalizi ya Bajeti ya Benki pamoja na utekelezaji wake, kuandaa mafunzo ya kitaalam kwa wafanyakazi wa Benki, kuratibu mfumo wa malipo ya kitaifa, yaani *National Payment System,* kusimamia utekelezaji wa mpango wa shughuli za Benki, yaani *cooperate plan,* kuandaa taarifa za fedha, yaani *Financial Statements.*

Tano, sifa za Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania zimetamkwa bayana katika Muswada. Kifungu cha 8(2) cha Muswada kimeainisha kwamba pamoja na mambo mengine, sifa hizo zilijumuisha angalua shahada ya kwanza, ujuzi na uzoefu usiopungua miaka kumi na tano katika fani ya Uchumi, Benki, Uhasibu, Fedha na Biashara na Sheria na awe ameongoza Taasisi au Idara za sekta hizo Serikalini, katika sekta binafsi au Mashirika ya Kimataifa.

Sita, akidi, yaani *quorum* ya Vikao vya Bodi kwa mujibu wa marekebisho ya Muswada kifungu cha 11(4) sasa itakuwa idadi ya Wajumbe sita badala ya watano na itatimia endapo Gavana ambaye ni Mwenyekiti kama hayupo nafasi yake itakasimiwa na

Naibu Gavana na Wajumbe wawili badala ya mmoja wanaotoka nje ya Serikali na nje ya Benki Kuu yenyewe watahudhuria Kikao.

Saba, Makatibu Wakuu wa Wazira ya Fedha, kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wataendelea kuwa Wajumbe wa Bodi ya Benki Kuu kutokana na nyadhifa zao, yaani *Exofficio Members* kwa mujibu wa kifungu cha 9(2)(c). Kutokana na hali hii, Muswada umebainisha katika kifungu cha 11(8) kwamba endapo Bodi itafikia maamuzi kwa kupiga kura, Makatibu Wakuu hawatapiga kura. Aidha, itakapotokea hali hii, Gavana anapaswa kutoa taarifa kwa Waziri wa Fedha. Hii ipo kifungu cha 11(10).

Nane, uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ambapo Gavana, Manaibu Gavana watatu pamoja na Wajumbe wanne wasio kuwa waajiriwa wa Benki Kuu au Serikali.

Aidha Muswada umeweka masharti katika kifungu cha 9(2) (d) kama ilivyorekebishwa kwamba anagalau Mjumbe mmoja kati ya wanne atatoka baina ya pande za Muungano.

Tisa, Benki Kuu kama Taasisi ya Umma, mahesabu yake yatakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma, yaani *The Public Finance Act, Cap. 348.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza yenye ibara ya kwanza mpaka tatu inahusu jina la Sheria, matumizi ya Sheria na ufafanuzi wa maeneo yaliyotumika katika Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Pili inahusu Ibara ya Nne hadi ya 24 ambazo zinatambua kuendelea kuwepo kwa Benki Kuu kama chombo kilichoanzishwa kisheria na kufafanua majukumu yake kuhusu Sera za Fedha, utoaji wa sarafu, usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha, kutunza dhamana za Serikali, kusimamia mfumo wa malipo na uwekezaji wa Hazina ya fedha za kigeni.

Sehemu hii ya Sheria pia inaweka wazi misingi ya uwajibikaji, uwazi na madaraka ya Benki Kuu katika utekelezaji wa majukumu yake, mashauriano baina ya Gavana wa Benki Kuu na Waziri wa Fedha kuhusu masuala ya Sera za Uchumi na Fedha, uteuzi wa Gavana, sifa zake, muda wa kuwa madarakani, uteuzi wa Manaibu Gavana, Wakurugenzi wa Bodi na wafanyakazi wa Benki pamoja na maslahi na stahili zao na taratibu za Vikao vya Bodi. Aidha, taratibu mpya zinazohusu hesabu na ukaguzi na masuala mengine ya utawala, yote yamezingatiwa katika sehemu hii ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inahusu sarafu na utoaji wake ambapo idhini ya Waziri wa Fedha inahitajika inapolazimu kutoa noti na sarafu mpya. Sehemu hii inahusisha ibara ya 25 hadi ya 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya Muswada yenye Ibara ya 31 hadi ya 61 inahusu shughuli nyingine za Benki Kuu. Shughuli zinazozungumziwa katika Sehemu hii zinahusu dhamana za Serikali, uwezo wa Benki Kuu kuuza na kununua dhamana zake kwa ajili ya utekelezaji wa Sera za Ujazi wa Fedha, utoaji wa mikopo kwa Serikali na utoaji wa mikopo kwa Mabenki na Taasisi za Fedha zenye matatizo ya ukwasi ambazo kuteteleka kwake kunaweza kuwa na athari kwenye mfumo mzima wa fedha nchini. Shughuli za Benki Kuu kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa Sera ya Ubadilishaji wa fedha za kigeni, yaani *Exchange Rate Policy*. Jukumu la Benki Kuu kuanzisha mfumo wa taarifa zinazohusu wateja wa Mabenki hususan kuhusu mikopo, utayarishaji na uchapishaji wa taarifa za urari wa malipo ya nje, yaani *Balance of Payments,* udhibiti wa shughuli za Mabenki na uwekezaji wa akiba ya fedha za kigeni ni baadhi ya mambo yaliyomo katika sehemu hii ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano na ya mwisho yenye Ibara ya 62 hadi 71, inapendekeza mambo mbalimbali ambayo ni pamoja na kinga kwa Wakurugenzi wa Bodi na wafanyakazi wa Benki Kuu, kinga kwa mali za Benki Kuu na zile zilizopo chini ya uangalizi wa Benki Kuu, kufutwa kwa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995 sura ya 197 na kumpatia Waziri mamlaka ya utekelezaji wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na hatimaye kuukubali kuupitisha kuwa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na uchumi baada ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa mwaka 2006, inayokusudia kufuta Sheria ya sasa ya Benki Kuu sura ya 197 ya mwaka 1995 kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu, hususan udhibiti wa mfumuko wa bei na usimamizi wa Sekta ya Benki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, ninaomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kwa kufanya kazi kwa masaa mengi na kwa uvumilivu mkubwa. Aidha, naomba kutoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Baraza la Wawakilishi kwa kukubali kuleta uwakilishi mzito wakati wa mjadala wa Muswada huu wakishirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Zakhia Meghji pamoja na wataalamu wa Wizara yake na Gavana wa Benki Kuu. Utaratibu huu ni mzuri kwa sababu unasaidia kuondoa tofauti zetu hususan tunapojadili masuala yanayohusu pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Hoogan, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Musa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

Wengine ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Ndugu Anselm Mrema ambaye ni Katibu wa Kamati na Ndugu Hellen Mbeba ambaye naye ni Katibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 70(2) toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Muswada ya Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 yanayokusudia kufuta Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995 na kupendekezwa kutungwa kwa Sheria Mpya ya Benki Kuu ili ikidhi matakwa ya mifumo ya uchumi iliyopo katika utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu hususan kuhusu sera ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalenga kuweka mifumo ya utendaji itakayotoa madaraka zaidi na kiwango kikubwa zaidi cha uwajibikaji na uwazi katika utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu inayozingatia taratibu zinazokubalika kimataifa katika utawala bora wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unazingatia mambo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, kufafanua majukumu ya Benki Kuu kuhusu Sera za Fedha, Sera ya Ubadilishaji wa Fedha na Usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha na mifumo ya malipo na uwekezaji wa Hazina ya fedha za kigeni.

Pili, kuweka misingi ya uwajibikaji na madaraka ya Benki Kuu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Tatu, muundo mpya wa Bodi ya Wakurugenzi, Kamati zake, uteuzi wa Wakurugenzi wa Bodi na mashauriano yahusuyo uchumi na fedha kati ya Benki na Wizara ya Fedha.

Nne, kuweka taratibu mpya zinazohusu hesabu na Ukaguzi wa shughuli za hesabu za Benki Kuu kulingana na taratibu za kimataifa.

Tano, kuweka taratibu za utoaji wa mikopo kwa Serikali, Mabenki ya Taasisi za Fedha zenye matatizo makubwa ya ukwasi ambazo kutetereka kwake kunaweza kuwa na athari kwenye mfumo mzima wa fedha nchini.

Mwisho, kuweka wazi jukumu la Benki Kuu, kuanzisha mfumo wa taarifa zinazohusu wateja wa Benki hususan kuhusu mikopo, utayarishaji na uchapishaji wa taarifa za uwiano wa mizania, yaani *Balance of Payments* na udhibiti wa shughuli za Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi imetambua na inatambua vyema mabadiliko makubwa yanayotokea kila siku katika mazingira ya kifedha na uchumi. Kamati inatambua kuwa shughuli za Benki Kuu zimeendelea kupanuka hasa kwenye maeneo ya Sera za Fedha na Mikopo, kuongezeka kwa mabenki na Taasisi za fedha nchini, mabadiliko ya umiliki ambapo sasa sekta binafsi inapewa kipaumbele na fursa kubwa katika uchumi wetu, msisitizo wa kuimarisha Benki za kuhudumia wananchi wa vipato vya chini kwa kuwapa mikopo midogomidogo, utandawazi unaosababisha mabadiliko ya teknolojia katika nyanja hususani shughuli za kibenki duniani kuelemea zaidi upande wa elekitroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya yanaifanya Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995 kutokukidhi na kutomudu mabadiliko haya kiutendaji na hivyo kuwepo na umuhimu wa kuibadilisha sheria hiyo. Kamati imeona kuwa suala la msingi ni Benki Kuu ikawa na uwezo wa kuongoza mabadiliko haya na si mabadiliko haya yaiburuze Benki Kuu, ndiyo maana nchi nyingi za Afrika kwa mfano Kenya, Zambia, Nigeria na zile za *SADC* au zimeshabadili sheria zao zinazotawala Benki Kuu au hivi sasa ziko katika mikakati ya kubadilisha sheria zao za zamani kuelekea katika mwelekeo niliouelezea hapo juu. Kwa utaratibu mabadiliko ya sasa ya mazingira ya Sekta ya Fedha sisi Kamati tumeona nasi Tanzania tusichelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala ya kuendesha uchumi wa nchi yetu, Benki Kuu ina jukumu kubwa la kusimamia sera za kifedha, yaani *Monetary Policies* zinazobuniwa kupangwa na kukubalika na Serikali kama inavyoainishwa katika Sera Kuu za Uchumi za nchi yetu *General Economic Policies.*

Wakati huo huo, Serikali ikisimamia Sera za Kodi na kuongeza akiba katika Mfuko Mkuu wa Serikali yaani *Consolidated Fund,* ni katika mantiki hii ambapo Kamati ya Fedha na Uchumi imeona ipo haja na umuhimu wa kutoa fursa na uhuru kwa Benki Kuu ili iweze kuendesha na kutekeleza jukumu la kusimamia Sera za Fedha na lile la usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha bila ya vikwazo kwa tija na ufanisi zaidi kwa

maana nyingine, lengo ni kuipa Benki Kuu uwezo na nguvu zaidi ya kumudu mabadiliko yanayojitokeza hivi sasa.

Kamati inatambua kuwa, kwa hali ilivyo sasa, kazi za Benki Kuu zinahitaji ufanisi kutoa maamuzi ya kila siku, kila wiki, kila mwezi na kila mwaka kwa maana ya kwamba majukumu hayo ni *decision intensive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu katika kuuchambua na kuutathmini Muswada huu wa Benki Kuu ya mwaka 2006 tuliweka msisitizo katika vifungu vinavyohusu utawala wa Benki Kuu na vile vilivyohusu usimamizi wa fedha na raslimali za Serikali. Suala kubwa lililojitokeza ni lile linalohusu dhana ya kuipa Benki Kuu uhuru wa kutenda shughuli zake.

Kamati ilipenda kujua uhuru huu ni upi hadi hatimaye kubaini kuwa uhuru unaozungumziwa hapa ni ule wa kuipa Benki Kuu uwezo wa kushughulikia vizuri zaidi usimamizi wa uendeshaji wa Sera za Fedha kama jukumu lake na vilevile kama mwajibikaji mkubwa wa matokeo ya utekelezaji wa sera hizo. Maana yake ni Benki Kuu kuwa na uwezo wa kutumia mamlaka ya kisheria, *instruments* zote ili kuwezesha taratibu nzuri za uendeshaji na usimamizi *(best practices)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhuru bila mipaka ni vurugu. Kamati yangu imeridhishwa na Muswada hasa ilipobaini na kuzingatia kuwa vifungu 73, 11(10), 21(1), 21(3), 21(4), 21(5) pamoja na 50(2) vya Muswada wa Sheria husika vinaonyesha wazi ni vipi Benki Kuu itawajibika kwa Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kikao cha Kamati kilichohudhuriwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Katibu Mkuu Hazina na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kilichofanyika tarehe 23-25 Machi, Kamati ilipitia vifungu vya Muswada huu. Baada ya majadiliano Kamati ilipendekeza marekebisho pamoja na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha Muswada huu ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri ameyakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pamoja na kuafiki kimsingi Muswada huu wa Serikali marekebisho na mapendekezo hayo mbalimbali ya Kamati yalikuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, kutokana na ukweli kwamba majukumu ya Benki Kuu yameendelea na yataendelea kupanuka, Kamati imekubaliana na pendekezo la kuwepo kwa Manaibu Gavana watatu katika uendeshaji wa Benki Kuu ili kumudu majukumu hayo. Lakini katika kulikubali pendekezo hili, Kamati ilishauri kazi za msingi za kila Naibu Gavana zijulikane na ziwekwe wazi ili sababu za kuwa na Manaibu Gavana hao wote ziwe wazi.

Pili, Kamati imeagiza Benki Kuu kufanya tathmini ya muundo wake wa sasa wa kiutawala na uendeshaji na ihuishe na ifanye maboresho ya muundo huo ili ulingane na kupanuka kwa majukumu ya Benki Kuu. Kamati pia imeagiza Benki Kuu itekeleze agizo hili mapema iwezekanavyo na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Kamati.

Tatu, Kamati ilishauri kwamba katika kutekelezwa majukumu yake ya Benki Kuu ya kusimamia Sera za Fedha, Gavana awe anashauriana na Waziri badala ya kutoa tu taarifa kwa Waziri inapogusa masuala muhimu ya Sera ya Fedha.

Nne, Kamati imeshauri kuwa Kifungu 9(2)(b) idadi ya Wajumbe wa Bodi ambao ni *Non Executive Directors* wawe wanne lakini ionyeshe wazi kuwa angalau mmoja atoke Zanzibar.

Tano, Kamati imependekeza katika kifungu 11(3) akidi ya Vikao vya Bodi iwe Wajumbe sita badala ya Wajumbe watano. Aidha, katika Kifungu 11(4) akidi ya Vikao vya Bodi itatimia endapo Gavana ambaye ni Mwenyekiti, kama hayupo nafasi yake itachukuliwa na Naibu Gavana na Wajumbe wawili ambao ni *Non Executive Directors* badala ya mmoja.

Sita, Kamati imekubali kuwa kifungu 11(5) ambacho kinampa mamlaka Mwenyekiti na Manaibu Gavana kufanya maamuzi katika masuala yatakayojitokeza kwa dharura kwa niaba ya Bodi, lakini Kamati imependekeza kuwa badala ya makubaliano ya maamuzi hayo ya dharura kusubiri Kikao cha kawaida cha Bodi ili itaarifiwe, Mwenyekiti aitishe Kikao cha Bodi mara moja ili awasilishe maamuzi hayo.

Saba, vifungu vinavyohusu uendeshajiwa wa mifuko ya fedha chini ya Benki Kuu kama vilivyoainishwa katika vifungu 18 pamoja na vifungu vyake vidogo moja mpaka nne vionyeshwe kwa uwazi zaidi vikizingatia Menejimenti ya mifuko hiyo na gawio la faida inayopatikana kwa wenye hisa.

Nane, Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wataendelea kuwa Wajumbe wa Benki Kuu kutokana na Nyadhifa zao *Exofficio Members* kwa mujibu wa kifungu 9(2)(c). Kutokana na hali hii, Muswada umebainisha katika kifungu cha 11(8) kwamba endapo Bodi itafikia maamuzi kwa kupiga kura, Makatibu Wakuu hawatapiga kura, Kamati imeridhia.

Tisa, Kamati imependekeza katika kifungu 5(1) kinachoonyesha majukumu ya Benki Kuu, Sheria hii itambue nafasi ya Benki Kuu katika kusimamia na kuendeleza Taasisi za Fedha zinazosimamia au zinazoshughulika na uwezeshaji wa Mtanzania wa Kipato cha chini, taasisi za mikopo ya nyumba na taasisi nyingine za kibenki ambazo lengo lake ni kushiriki katika kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuujadili Muswada huu Kamati yangu vilevile ilikuwa na maoni ya jumla kwa Serikali yafuatayo:-

(i) Kamati imesisitiza muundo wa Benki Kuu kuendelea kurekebisha muundo wa Sera ya Fedha hasa tukizingatia matakwa ya Awamu ya Pili ya mageuzi katika Sekta ya Fedha;

(ii) Kuimarisha Taasisi na taratibu za kisheria ili kuondoa vikwazo vya utoaji wa mikopo na kuboresha huduma za sheria na mahakama;

(iii) Kuboresha usimamizi wa mfumo wa fedha ulio madhubuti na wenye ufanisi;

(iv) Kuendeleza masoko ya fedha yenye ufanisi wa kuboresha miundombinu na utendaji wake;

(v) Kuimarisha Sekta ya Pensheni na Bima;

(vi) Kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Mikopo Midogo Midogo;

(vii) Kuweka na kuendeleza miundombinu ya Sheria na Mahakama;

(viii) Kutunga sera na taratibu za kisheria kuhusu utoaji wa mikopo ya muda mrefu ya maendeleo ili kuziba pengo lililopo katika utoaji wa mikopo ya muda mrefu kwenye Sekta za Uzalishaji;

(ix) Kuanzisha mpango wa kudhamini mikopo ya muda mrefu ya maendeleo; na

(x) Kuanzisha Taasisi ya kutoa mikopo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao makini *(constructive criticism)* ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Naibu wake; Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, Gavana wa Benki Kuu; Ndugu Daudi Balali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja pamoja na maafisa wote wa Benki Kuu. *(Makofi)*

Aidha, shukrani za pekee zinatolewa kwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Mwinyihaji Makame, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Ndugu Meza, pamoja na Maafisa wao na Wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Ame Mati Wadi na Mheshimiwa Salmin Awadhi Salmin, kwa kusaidia Kamati kufanikisha kujadili na kupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako naomba niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Benki Kuu *(The Bank of Tanzania Act, 2004).*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha maoni hayo kutokana na kifungu cha Kanuni Na.43 (5)(b)(c) na kifungu cha 81(1) toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia ndani ya Muswada wenyewe naomba awali ya yote, kumpongeza Waziri wa Fedha na timu ya wataalam wake wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kutayarisha vyema Muswada huu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Kamati ya Fedha na Uchumi (Haidhuru Wajumbe wote watatu waliokuja walitoka Chama Tawala, labda Spika Kificho alisahau kuwa katika Wajumbe wa Kamati yake pia wapo wa Chama cha Upinzani) wakishirikiana na Waziri wa Nchi anayehusika na Wizara ya Fedha pamoja na Naibu Katibu Mkuu wake.

Aidha, napenda kumpongeza Gavana na timu yake kwa kumsaidia sana Waziri na Kamati katika kufafanua vifungu mbalimbali ambavyo vilionekana kuwa na utata wakati wa kujadili Muswada wenyewe. Pia, tunawapongeza kwa kutupatia nyaraka mbalimbali ambazo tulizihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu ulioanzishwa na Kamati yetu ya Fedha na Uchumi wa kuwaalika wenzetu kutoka Zanzibar wakati wa kujadili Miswada ambayo hatimaye itakuwa Sheria itakayotumika katika pande zote za Jamhuri ya Muungano. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani ndio njia muafaka itakayoweza kupunguza kwa kiwango kikubwa manung'uniko na hata kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Muungano, ilimradi kila upande upate fursa sawa wakati wa kuwasilisha hoja, isionekane kuwa kuna mkubwa na mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati ikiupitia Muswada huu yalijitokeza mambo yafuatayo, ambayo Kambi ya Upinzani inaona ni vyema kwa Wabunge na wananchi wayaelewe.

(i) Kuweka kumbukumbu;

(ii) Kuona mafanikio na mapungufu yaliyopo ili tujipange vizuri katika hii Awamu ya Nne ya Serikali yetu ambayo moja katika mipango yake ni kuimarisha Muungano wetu kwa lengo la kuondoa kasoro za kimfumo na za kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Benki Kuu yetu ilianzia pale ilipovunjwa *East African Currency Board* ambayo ilikuwa ikimilikiwa na Aden, Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo miaka ya 1964/1965 iliamuliwa kuvunjwa Bodi hiyo ya sarafu ili kuziwezesha nchi hizo za Afrika ya mashariki kusarifu uchumi wa kila nchi kwa mujibu wa mazingira mapya ya kuwa nchi zetu zimepata uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uamuzi huo kila nchi ilirejeshewa fedha zake ilizoziweka katika Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki kwa mpango ufuatao: -

(i) Mtaji *(Paid up capital);*

(ii) Gawio la mafao *(Dividends);*

(iii) Michango na ada za uanachama wa *IMF* na *ADB* kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgawanyo wa hisa zilizokuwa *East African Currency Board,* Tanganyika ilipata asilimia 88.95%,Zanzibar ilipata na asilimia 11.05% na asilimia hii ya hisa ndio ulikuwa mtaji wa Zanzibar katika uanzishwaji wa Benki Kuu tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tokea mwaka 1965 hadi mwaka 1993 Zanzibar haikuwahi kupata gawio la faida kutoka Benki Kuu ya Tanzania japokuwa iliweka mtaji wa asilimia 11.05%. Hali hiyo ilionekana kuwa ni kasoro kubwa, hivyo basi mazungumzo ya pamoja ya Serikali mbili yalifanyika na kukubaliana kuajiri Shirika la Fedha la Dunia *(IMF)* ili kuchunguza mambo yanavyotakiwa kuwa baina ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti hiyo ya *IMF* ndio chanzo cha Zanzibar kupata gawio kuanzia mwaka 1994 baada ya *IMF* kutengeneza utaratibu wa muda wa 4.5% ndio Zanzibar imepata jumla ya Shilingi bilioni 3.7 kutoka mwaka 1994 hadi 2004, kati ya jumla ya Shilingi bilioni 82 zilizotakiwa kugawiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa katika hali hii haiwezekani kusiwe na manung'uniko katika uendeshaji wa Benki Kuu. Pamoja na kasoro hiyo kubwa hadi leo hata ile *formula* ya muda ya 4.5% ambayo imekwishadumu zaidi ya miaka 10 haijafanyiwa masahihisho, jambo ambalo limesababisha Zanzibar kuona kuwa inazidi kupunjwa katika mgao wa faida baina yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia hisa za asilimia 11.05 za mwaka 1965, ni dhahiri kuwa hisa hizo kwa hesabu za sasa mgao ungekuwa umebadilika hasa tukitilia maanani kuwa katika kipindi cha miaka 30 (1965 - 1994) Zanzibar haikupewa gawio hata mwaka mmoja, wala haijui ni kiasi gani cha gawio ilistahili kupata. Haya ndiyo mapungufu ambayo Rais Kikwete anataka yarekebishwe ili Muungano wetu uzidi kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika historia ya uchumi wetu, hadi mwaka 1984, Zanzibar ilikuwa na akiba zaidi ya fedha za kigeni kuliko Serikali ya Jamhuri na ndio

maana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliweza kununua ndege za kivita *Mig 27* wakati wa Marehemu Karume, mizinga ya masafa marefu na mafupi na silaha nyingine kadhaa.

Pia iliweza kulisaidia Jeshi la Polisi katika mahitaji ya vifaa vyake hasa magari na Ofisi, pamoja na kwamba huduma hiyo ilitakiwa ifanywe na Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile dhana ya kuwa mgao wa gawio la Serikali ya Muungano kwamba ilikuwa katika matumizi pia ya kuisaidia Zanzibar sio sahihi, kwani ni wajibu wa Serikali ya Muungano kuvihudumia vyombo vyote vilivyo ndani ya mfumo wa Serikali ya Muungano na sio msaada. Msaada utakuwa kwa vyombo visivyo vya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, katika Bunge la Bajeti lijalo ni vyema Serikali ikaja na taarifa rasmi juu ya mgawanyo sahihi wa hisa katika Benki Kuu na hasa kwa sasa kwa vile mtaji unabadilika na unatokana na fedha za *BOT* siyo wenye hisa ili kuondoa manung'uniko yasiyo na sababu. Sambamba na hatua hii, tunadhani pia Kamati ya Pamoja ya Fedha ije na *formula* ya mgawanyo wa mapato na matumizi ya Jamhuri ya Muungano, kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri na ile ya Zanzibar, ili kama alivyosema Rais Kikwete kuwa tumalize matatizo haya kwa kuweka misingi imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba chombo hiki ni mali ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo basi itakuwa ni vyema katika muundo wa Benki Kuu kuonyeshwa wazi mgawanyo wa ajira baina ya pande mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu unatokana na hali halisi ilivyo hivi sasa, kwani zaidi ya asilimia tisini na saba ya watumishi wa chombo hiki wanatokea katika sehemu moja tu ya Jamhuri.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kuwa katika uhai wote wa Benki Kuu (miaka 40) wameshindwa kupata hata mtu mmoja anayeweza kuwa Mkurugenzi wa Kitengo kutoka Zanzibar. Hili ni la utendaji linaweza likashughulikiwa pakiwa na nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kwa kifupi sana nitoe maoni ya Kambi katika baadhi ya vifungu vya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haina sababu za kuupinga Muswada huu ila ina mapendekezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona umuhimu wa Muswada huu na inaelewa matakwa ya nchi katika ukuaji wa uchumi na umuhimu wa kusimamia vyema mfumuko wa bei, riba na ujazi wa fedha. Aidha, Kambi inaelewa namna Vyombo vya Fedha vya Kimataifa kama *World Bank* na *IMF* wanavyopenda kuona kuwa mabenki ya dunia ya tatu yanakua ili yalingane na yale ya mataifa tajiri hatua kwa hatua. Pamoja na kuelewa hayo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuzidi kuwa makini katika

kubadili mifumo ili tusije tukaingia kwenye mtego. Aidha, ni vyema Serikali ikashirikiana na Bunge katika mchakato mzima wa kuleta mabadiliko katika Asasi zetu ili wananchi wetu wayapokee mabadiliko hayo bila ya wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tano inayohusu *Principal Functions of the Bank,* tunaonelea kuwa uchumi wa nchi yetu unategemea kwa kiasi kikubwa utendaji wa vyombo vinavyotoa mikopo kwa wananchi. Hivyo basi, ni bora ikatajwa wazi kuwa moja kati ya kazi kuu za Benki Kuu iwe ni kupanga viwango vya riba zitolewazo na Benki za Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Gavana juu ya tatizo la kudhibiti riba, hivi sasa ukichukua mkopo riba na *Bank Charges* ni wazi mabenki yanawanyonya wateja kwa kiwango cha juu sana. Kwa njia hii, vyombo vinavyotoa mikopo hasa mabenki ni wazi matajiri watazidi kutarijika kwa kupewa mikopo yenye riba ndogo eti wao wanakopesheka na mkulima ataendelea kurudi nyuma kimaendeleo eti yeye hakopesheki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ibara ya nane inayohusu uteuzi wa Gavana na Manaibu wake, kifungu cha 8(3) kinasema: "Rais atawateua Manaibu Gavana watatu."
Lakini tungependa kusema kuwa, pamoja na kwamba baada ya mchakato na kuelezewa mambo mengi na hasa kupewa kwa kina utendaji wa kila Naibu Gavana, tungependa basi kusisitiza kwamba suala la gharama za kuendesha Benki lichunguzwe sana. Kwa sababu hiyo itapunguza gawio la wenye hisa na hilo si jambo zuri sana. Kwa maana hiyo, tunakubaliana na pendekezo hivi sasa baada ya kupata mchakato huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 8(1) kinachohusu uteuzi wa Gavana na Manaibu wake, ukiangalia uwezo wa uamuzi alionao Gavana, ni dhahiri tu Bodi inaweza kuwa dhaifu katika kutoa maamuzi. Hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa Wajumbe wa Bodi wawe watano badala ya wanne kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada kwa vile Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mapendekezo haya hawapigi kura.

Mheshimiwa Spika, wakati ule tulikuwa na Wajumbe 10 katika Bodi ya Benki Kuu na wote walikuwa na uwezo wa kupiga kura. Wakati ule vile vile, Katibu Mkuu wa Hazina na Katibu Mkuu wa Zanzibar, hasa Katibu Mkuu wa Hazina wa Jamhuri ya Muungano alikuwa na Kura ya *Veto* katika Bodi, lakini sasa hivi hawana kura. Kwa hiyo, hiyo imepunguza nguvu ya wenye hisa kusimamia vizuri chombo hiki. Lakini kutokana na mapendekezo yaliyokuja hivi sasa inaonekana wazi kwamba Gavana akikaa yeye mwenyewe na Manaibu wake wanne wanaweza kutoa maamuzi na kama ikiwezekana kumpata tu Mjumbe mmoja wa Bodi. Kwa hiyo, sisi tunashauri kwamba, badala ya Wajumbe wanne waliopo, wawe watano ili angalau wawili waweze kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaji wa Benki Kuu sasa utakuwa Shilingi bilioni moja kutokana na kifungu cha 17(1) kwa kulinganisha na Sheria ya *BoT*, 1966 ibara ya

14(1) iliyokuwa inasema ni Shilingi milioni 20 na Sheria ya *BoT* ya 1995 bilioni 10 fedha za Kitanzania. Kambi ya Upinzani inadhani huu ni mtaji ambao uliwekwa na pande mbili za Muungano. Hivyo basi, kuna umuhimu wa kuonyesha mgawanyo wa kiasi ambacho kimetolewa na kila upande. Kwa jinsi hii itapunguza malalamiko na manung'uniko ya mgawanyo wa faida na hasara zinazopatikana katika utendaji kazi wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine mengi Waheshimiwa Wabunge wameyaongelea katika Semina iliyofanyika katika ukumbi huu tarehe 28/03/2006, hivyo itakuwa sio busara kuyarejea ila ninatarajia kuwa yatasahihishwa pindi Muswada huu utakapopitishwa na kuwa Sheria ya Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani tupate ufafanuzi wa yale niliyoyasema, lakini pia tunaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mbele yetu tuna majina ya wachangiaji kumi. Kwa hiyo, nafasi bado zipo kwa wengine ambao wanafikiria wanaweza kuomba kuchangia. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Elisa David Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Mheshimiwa Rished Abdallah ajiandae.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache katika Muswada huu wa Benki Kuu ya Tanzania uliopo mbele ya Bunge lako Tukufu *(The Bank of Tanzania Act, 2006)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake pamoja na watendaji wake wakuu kwa kuandaa Muswada huu wa Benki Kuu na kuuleta hapa Bungeni na kuuelezea kama inavyopasa. Nawapongeza sana. Muswada huu kama ulivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha una madhumuni na nia ya kuipa uwezo na madaraka makubwa Benki yetu Kuu ya Tanzania ili iweze kutenda na kuendesha shughuli zake kwa umahiri zaidi na kwa uhuru zaidi ikitumia sheria hii na kukidhi mahitaji ya vyombo mbalimbali ambavyo vipo yaani Mabenki na Taasisi za Fedha katika Sekta ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inawapa madaraka zaidi ya kisheria na kiwango cha kutenda kazi zao na kiwango kikubwa cha uwajibikaji wakitumia au wakitenda kazi zao kwa uwazi zaidi na wakitumia mifumo mbalimbali ya teknolojia iliyopo katika Sekta ya Fedha sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka 15 iliyopita tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika hii Sekta ya Fedha hapa nchini. Kumeanzishwa mabenki takriban 25 na maduka ya kuuza na kununua fedha za kigeni *(Bureau de Change)* karibu 120. Mabadiliko haya ni makubwa sana na vyombo hivi vimeanzishwa kukidhi haja kubwa ya

huduma za kibenki na huduma za kifedha ambazo zimeibuka katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo hivi vya fedha vinahitaji usimamizi mkubwa. Vyombo hivi vya fedha vimekuwa na sera ambazo wakati mwingine hazikuendana na sera za fedha za nchi yetu. Vimekuwa vikisaidia kweli kuendesha ama pia kusaidia uchumi wa nchi yetu kwa kukopesha na kwa kutoa fedha zinazohitajika kuendesha uchumi, lakini vimekuwa na malengo tofauti katika nyakati mbalimbali. Kwa mfano, tukitazama sera zao za fedha, *interests* wanazo-*charge* zilikuwa kubwa sana na watu wengi waliokopa kutoka kwenye mabenki haya na Taasisi hizi za fedha wamekuwa wakilalamikia riba hizi.

Aidha, mabenki haya pamoja na Taasisi hizi mbalimbali za fedha zilizoanzishwa zimekuwa zinaendesha shughuli zao katika sehemu za Mijini tu, hazijapeleka huduma zao za kibenki au za kifedha katika sehemu za Vijijini katika nchi yetu. Hivyo, wanavijiji, wakulima ambao ndiyo watu wengi katika nchi yetu hawakufaidi na wataendelea kutofaidi huduma hizi za kibenki ambazo zimeanzishwa. Hii inahitaji usimamizi mkubwa. Vyombo hivi vinahitaji usimamizi mkubwa wa Benki Kuu na mimi nafikiri kwa hatua hii tunayoichukua sasa, kwa sheria hii tunayoipitisha, itawawezesha Benki Kuu kuwasimamia hawa wenye vyombo hivi na Taasisi hizi za fedha ili huduma hizi ziende mpaka Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya matukio mbalimbali ambayo yametokea hasa niki-*quote* kufilisika kwa mabenki mawili hapa nchini, Benki ya *Meridian Biao* na Benki ya *Greenland*. Benki hizi ni kati ya Taasisi zilizoanzishwa hapa nchini ili kukidhi haja ya kutoa huduma za kibenki. Vyombo hivi havikusimamiwa vizuri na wenyewe na mwisho wake vimefilisika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi kusikia kwamba Gavana wetu jana alituambia kwamba hapakuwepo na madhara makubwa yaliyotokea kutokana na kufilisika kwa haya mabenki mawili. Hakuna mteja, hakuna Mtanzania aliyepoteza amana zake. Lakini kama Gavana alivyoeleza jana, bado inawezekana mabenki haya ambayo yameanzishwa yakaweza kufilisika na yakifilisika labda kutatokea madhara makubwa kwa wawekezaji katika mabenki hayo. Hivyo, kwa kuwapa Benki Kuu uhuru wa kuendesha mambo yao kwa uwazi zaidi, kwa utaalamu zaidi, kwa kutumia mifumo mbalimbali na teknolojia ambayo ipo sasa katika Sekta ya Fedha, wanaweza wakasimamia mabenki haya ili yakaendeshwa vizuri na tusiwe na madhara ambayo yametokea huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie matazamio yangu katika uanzishaji ama kupitisha sheria hii ya kuwaruhusu Benki Kuu kuwa huru zaidi. Tumeelezwa kwamba, sasa hivi Benki Kuu licha ya shughuli zake, katika *section 5(2)* kumeainishwa *Second Generation of Financial* ambazo tunazitarajia katika nchi yetu nazo ni uanzishaji wa Benki ya Maendeleo, Benki ya Nyumba, Benki ya Kilimo, Benki ambayo itakuwa inashughulika na *equipment leasing* pamoja na kusimamia miradi mikubwa mikubwa ambayo tumekwishaanzisha hapa nchini ambayo ni *Vision 2025, Millennium Development Goals* na *Poverty Reduction.* Nafikiri kwamba kwa uwezo ambao

tutawapa Benki Kuu kwa sheria hii wataweza kusimamia zaidi na kwa ukaribu uanzishaji wa *Second Generation Financial Reforms* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naomba niseme naunga hoja hii mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni Muswada wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali kuwa dunia imebadilika, ulimwengu umebadilika kwani miaka 10 iliyopita nyuma siyo sasa. Sekta zote zimeendelea kupanuka kimaendeleo na kiteknolojia zikiwemo Sekta za Kijamii, Sekta za Kiuchumi na Sekta za Kifedha. Ukuaji wa Teknolojia ya Upashanaji Habari *(Information Technology)* umefanya ulimwengu huu kuruka kimaendeleo. Kwa maana hii na sisi Tanzania ni lazima tujiweke sawa ili twende sambamba na mabadiliko haya.

Kwa maana hiyo, ndiyo maana Muswada huu leo uko hapa kwa kuujadili ili uweze kwenda sambamba na hayo mabadiliko ingawa majukumu ya Benki Kuu yamebakia yale yale ya kuhuisha uchumi kwa maana ya ku-*regulate* kupitia sera za kifedha na *instruments* zake, yaani *Monetary Policies and Monetary Policy Instrument,* lakini Sekta ya Fedha imepanuka. Tanzania tunaona kuwa mabenki mengi yameanzishwa, *Bureau de Changes* mbalimbali zimeanzishwa, kwa hiyo ni lazima chombo hiki kipewe uhuru wa kutosha wa kuweza kufanya kazi zake ili mambo yaende sawia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu wa jumla jumla naona bora nijikite kwenda katika vifungu mbalimbali vya huo Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, page 31, *section 8(2)(b)* imezungumzwa pale kwamba unahitajika uzoefu wa miaka 15 katika *field* za uchumi, fedha na mabenki kwa mtu kuchaguliwa kuwa Gavana. Muda huo naona kama ni mwingi na utawanyima vijana kuingia pale katika Benki kuwa Magavana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua umri wa kusoma kutoka Darasa la Kwanza mpaka *Ph.D,* basi angalau ni miaka 21. Pale kunakuwa na *interval* baina ya *level* moja ya *education* na *level* nyingine na angalau basi kutakuwa na *interval* ya miaka saba. Halafu ukichukua kama mtu anaanza Darasa na Kwanza akiwa na umri wa miaka saba kwa hesabu za haraka haraka mtu anatakiwa awe na umri wa miaka 50 na kuendelea ili awe Gavana na akifika hapo baada ya muda mfupi inabidi astaafu. Naomba suala hili lifikiriwe sana, huu uzoefu upungue uwe ni miaka 10 kwa sababu mtu akifanya kazi yake kisawasawa miaka 10 atakuwa na uzoefu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la *Deputy Governors* watatu. Kwa ghafla ghafla tu kutoka mmoja kwenda watatu utaona ni wengi mno, lakini kuna *justification* ya kutosha. Kama kutakuwa na mgawanyo wa kazi vizuri utaepusha

mwingiliano baina ya kazi za mmoja na mwingine. Hata ilivyoainishwa kuwa katika *Deputy Governors* watatu hao angalau mmoja basi atokee Zanzibar na kwenye *amendment* imeonyesha hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *section* namba 9(2)(d) kuna *Non Executive Directors* wanne ambao watachagulliwa na Waziri wa Fedha. Mimi napendekeza basi, ilivyokuwa namba ni nne, basi wawili watoke upande mmoja wa Muungano na wawili watoke upande mwingine badala ya mmoja kutoka upande wowote ule.

Kwa maana hiyo, kwa hesabu ya haraka haraka, wapigakura hawa ni 10. Tukichukua hesabu ya mmoja katika wale watatu na wawili watatoka Zanzibar ambao ni *Non Executive Directors* na mmoja ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Zanzibar. Kwa hiyo, tutakuwa na Wajumbe wanne kutoka Zanzibar na Wajumbe sita kutoka Muungano au *vice versa* kwa sababu inaweza ikawa upande huu au ikawa upande ule. Kwa maana hiyo, upande mmoja utakuwa na kidogo kuliko upande mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *page 33 section (9)(1)(a)*, pale kuna suala la *disqualification for appointment to the board* kuwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawastahiki kuwa Wajumbe wa Bodi hii ya *BoT*.

Kwa hiyo, hapa ningependa tu tupewe sababu kwa nini ikawa hivyo kwa sababu humu mna wataalam waliobobea, wana uzoefu wa kutosha katika *field* hiyo na wanaweza wakafanya kazi nzuri ya kutetea maendeleo ya Benki Kuu na Sekta ya Fedha, lakini hapa tunaambiwa hawastahiki. Tupewe sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *section 9 (1) (d)* imezungumza kwamba *office bearers* wa Vyama vya Siasa hawastahili kuwemo katika hiyo bodi, nakubaliana na hili moja kwa moja. Lakini nataka iongezwe pale imeandikwa vyama vilivyosajiliwa, mimi nataka iongezwe vyama vya siasa vilivyosajiliwa na visivyosajiliwa kwa sababu wakiingia kule kwenye vile vikao pengine wanaanza kuanzisha mapambano ya kisiasa mle ndani, hawa nakubali wasiwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *page number 34 section 11 (5),* inasema ili kuondoa Naibu Gavana watatu peke yao kufanya uamuzi wa yale masuala yaliandikwa *unusually urgent nature* kwa sababu kama Mwenyekiti hayupo ambaye ni *Governor, Deputy Governor* ambaye ni *Deputy Chairman* anaweza akawaita ma-*deputy* wake wawili wakawa ma-*deputy* watatu kwa maana hiyo wakafanya huu uamuzi. Halafu uamuzi ule unachukuliwa kama ni uamuzi wa bodi uliotimia *quorum* na wajibu *report* katika *next regular meeting* itakayoitwa baada ya maamuzi haya. Lakini mimi ningeshauri kuwa kikao kifanyike watoe maamuzi lakini maamuzi yachukuliwe kama ni maamuzi ya *management* tusiitwike bodi maamuzi ambayo wao wenyewe hawakushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *page 34 section (1) (6),* inaeleza kuwa maamuzi ya vikao yafanyike kwa *consensus* sawa na kama haikuwezekana basi kura zipigwe. *Definitely* kwa hesabu tulizotoa kuwa kuna upande mmoja kutakuwa na wajumbe

wachache katika pande hizi mbili ikipigwa kura kwa vyovyote wengi watashinda. Hapa imeambiwa matokeo ya uchaguzi na maamuzi hayo yaliyopitishwa kwa uchaguzi apewe taarifa Mheshimiwa Waziri Fedha. Sawa lakini je, hawa wengine ambao walikuwa hawakukubaliana hawana sehemu ya kukata rufaa na sababu zao kwa nini wakakataa zile rufaa zikasikilizwa au ni huyo huyo Waziri wa Fedha, atapokea hiyo rufaa na kama hivyo basi iainishwe kwenye bodi kwa sababu chombo kinaendeshwa na binadamu na binadamu tuna mapungufu inaweza ikatokea vuta nikuvute ikatokea namna hiyo. Kwa hiyo, wajue wapi wanaweza kwenda kukata rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *page 39 section 18 (4),* jana Mheshimiwa Gavana alipokuwa anajibu suala la mgawanyo wa faida Benki Kuu upande wa Bara na Zanzibar alipoulizwa ile asilimia 4.5 na kwa nini isiwe asilimia 11 ambayo ni *share* ya mtaji Zanzibar iliyochangia katika kuunda Benki Kuu, alijibu hayo ni makubaliano na tunakubali *IMF* ilikuja ikatoa ripoti yake ikapendekeza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa alieleza ile tofauti ambayo ni 6.5 inatumika kwa ku-*finance* shughuli za kimuungano. 6.5 ni tofauti ya baina ya 11% - 4.5% ambayo wanapatiwa sasa Zanzibar. Hili nataka kujua ni jibu la uhakika? Yapo makubaliano hayo? Je, kama ni sahihi, Watanzania wanaelewa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama ni hakika na inakwenda hivyo 6.5% ya *share* ambayo ilikuwa iende *direct to* Zanzibar inakuja ku-*finance* matumizi ya Muungano basi iweke sawa tujue mchango wa Zanzibar kwenye Muungano ni huu 6.5% na *trend* yake ionekane tokea hapo ilikuwa ni kiasi gani ambacho kinachangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho ni *page 53 section 52(1),* inazohusu *BOT* ku-*deal* na mambo ya dhahabu kuuza, kuingiza kufanyaje kwa hiyo, labda hii tuweke sawa hii shughuli inaendaje katika Benki Kuu sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa niunge mkono hoja iliyopo mbele yetu. Niipongeze Kamati pamoja na Serikali kuleta huu Muswada japokuwa tumechelewa sana katika masuala ya fedha kulingana na hali halisi ya ulimwengu jinsi tunavyokwenda. *(Makofi)*

Vile vile mimi naamini kwamba tusingekwenda sambamba na Muswada huu pengine tungepoteza mambo mengi kutoka Benki ya Dunia na *IMF.* Pamoja na kwamba haya ni moja ya masharti ambayo wakubwa wanataka tuwe pamoja nao lakini Muswada huu ni moja ya masharti ya Benki ya Dunia pamoja *IMF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maoni yangu kwa hiyo, hatuna budi kutokana na hali halisi ya *globalisation.* Tusipofuata tutapoteza mambo mengi na ndiyo dunia sasa hivi inakokwenda. Mimi nataka kuzingatia zaidi kuzungumzia *role* ya Benki Kuu katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakua kiuchumi. Sasa hivi tatizo kubwa la Watanzania ni kukosa mitaji. Kukosa huku kwa mitaji ni kwa sababu ya umaskini tuliokuwa nao lakini

na hicho kidogo ambacho kipo Benki ina nafasi kubwa kuweza kusimamia na kuhakikisha kwamba Taasisi za Fedha kama Benki wanazisimamia vizuri na kuweka masharti nafuu na masharti hayo yatekelezwe ili Watanzania wapate mitaji na kujiendeleza kiuchumi. Sasa hivi nchini tunaambiwa tuna Benki 32 lakini ukilinganisha Benki ambazo ziko *serious* ziko 7 au 8 zingine ni ndogo ndogo au ni Taasisi za Fedha ambazo hazina misuli mikubwa ya kuweza kukidhi haja ya kuwakopesha Watanzania walio ngazi ya chini. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hizi Benki ambazo kidogo zinaweza zikatoa mikopo mizuri wana masharti magumu, *interest rate* zao ni kubwa ambazo Mtanzania wa kawaida hawezi akazimudu. Lakini wanapokopa wewe, *interest* ukaweka fedha katika *fixed deposit* wanakulipa asilimia 5, 6, kutegemea na Benki zinavyoeleza masharti yake. Lakini wewe ukichukua fedha Benki basi *interest* yake inaanzia asilimia 16 na kwenda juu. Sasa kwa kweli uwiano hapa ni mbaya sana kwamba wewe ukichukua fedha Benki inabidi ulipe riba kubwa na wewe ukiweka fedha zako Benki wanakupa riba ndogo. *(Makofi)*

Sasa mimi nafikiri Benki Kuu inaweza ika *play a very big role* kusimamia Benki hizi na kuwe na majadiliano mazuri ni jinsi gani tuwawezeshe Watanzania waweze kukopa fedha, fedha ziko nyingi kwenye mabenki na tunaambiwa kwamba hakuna wanaokwenda kuzikopa ni makampuni ya kigeni ambayo yanakuja ku-*invest* hapa na sisi tunabakia kuajiriwa katika baadhi ya nafasi za Mashirika hayo lakini hatufaidiki kabisa na mfumo mzima wa mzunguko wa fedha katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ningeliomba Benki Kuu, kulisimamia kwa nguvu sana kwa sababu ya shughuli za maendeleo na hasa ukizingatia ya kwamba uchumi mkubwa wa nchi hii ni kilimo. Benki zinatoa mikopo mikubwa kwa ajili ya shughuli za biashara. Lakini biashara hizo hizo zinaweza zikawa ni nzuri ikiwa kilimo kitaendelezwa kutokana na *product* zinazotoka katika mashamba kama pamba, kahawa, chai na korosho na viko vitu vingi sana na hata katani ambayo ni mazao ambayo yakiingia kiwandani hatimaye mfanyabiashara na yeye atafaidika. Lakini kama mazao hayo hayatapewa kipaumbele katika kupewa mikopo wanaoshughulika na mambo kama hayo, sasa tunakwenda katika *scale* ya chini kwamba kila Mtanzania azalishe ili kukuza uchumi na yeye ajiendeleze. Hawezi akajiendeleza kama hawezi kupata mikopo.

Sasa tutazame vile vile Benki Kuu, ni jinsi gani itaweka mikakati pamoja na Serikali na Benki ambazo zitaweza kuwakopesha wakulima na hatimaye kukuza uchumi huu. Tuna matatizo mengi ya kukua kwa uchumi, ukiachilia mbali matatizo ya umeme ambayo *tariff* yake bado ni kubwa, masharti mengi ya biashara bado ni magumu. Lakini *at least* basi pale panapokuwa na uwezo wa kuzalisha kwa wingi kwa wananchi wa kawaida na hatimaye ndiyo tutaweza kukuza uchumi. Sasa hivi nchi yetu inakua kutokana na hawa wakulima wadogo wadogo. Sijaona kama kuna ukulima mkubwa ambao umeiwezesha Tanzania kuweza kuonekana kwamba mazao haya au katika shamba hili kubwa limeweza kukuza uchumi wa nchi isipokuwa ni kutokana na wakulima wadogo wadogo. Sasa lazima tuwape kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapochukua mkopo ndiyo yale masharti tunayopata kutoka Benki. Tuwe na utaratibu wa mtu kukopa na hatimaye kuweza kujenga nyumba. Sasa hivi tuna utaratibu wa kukopa kuwasomesha watoto shule. Hiyo haitoshi, tunataka vile vile tukope ili tuone tunafanyaje katika kujiendeleza.

Lingine labda niulize swali hivi hii migodi ya dhahabu ambayo sasa hivi imeanza kuibuka nchini mimi nina hakika migodi hiyo ya dhahabu inaweza ikaifanya Benki Kuu kuwa na nguvu katika *reserve* zake. Hivi itachukua muda gani ionekane kwamba migodi ya dhahabu au *product* zinazotoka katika migodi ya dhahabu zinachangia kwa kiwango kikubwa kuonekana kwamba sarafu yetu ya Tanzania sasa ina nguvu kwa sababu jinsi sarafu yetu inavyoshuka kila siku kwa kweli hairidhishi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu inaweza ikadhibiti kwa uzuri zaidi. Lakini maelezo tunayopewa ni ya kitaalam mno ambayo mwananchi wa kawaida ukimwambia kwamba sarafu ya Tanzania inashuka thamani lakini uchumi umekuwa, hakuelewi. Sasa hii lazima itafsiriwe kwa vitendo kwamba sarafu ndiyo inashuka lakini uchumi unakua wakati akinunua kilo moja ya sukari, mwezi uliopita ilikuwa shilingi 600 baada ya mwezi mmoja inakuwa shilingi 800 halafu unamwambia uchumi umekua yeye anakuwa haelewi. *(Makofi)*

Sasa Benki Kuu bado ina dhamana kubwa katika nchi hii kuhakikisha kwamba inadhibiti uchumi wetu usiende kiholela na hatimaye tuweze kunufaika kwa upana wake ili mwananchi aweze kufaidika na nchi yake mwenyewe katika kukopa, hawezi mtu kujiendeleza kama hawezi kukopa Benki na hili limekuwa ni kikwazo kikubwa kwa Watanzania, sasa hivi tunajaribu kuwahamasisha wananchi wetu kuunda *SACCOS.* Sasa hivi tunaona kuna utaratibu wa Serikali ambao umeleta utaratibu *SME's* kuwakopesha wafanyabiashara ndogo ndogo na wa kati. Lakini bado inachukua muda mrefu katika utekelezaji wake.

Sasa sijui labda baada ya kupitisha sheria hii Benki Kuu itatoa mchango gani kwa Benki ambazo zinataka kuwakopesha wananchi hawa ili na wao wajiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia *role* ya Benki Kuu ni jinsi gani itatusaidia wananchi wadogo wadogo waweze kukopa na wao wajiendeleze na hatimaye Benki Kuu iwe na nguvu zaidi katika kuendeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nishukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Gavana na timu yake kwa kuweza kuleta Muswada huu hapa Bungeni. Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka. Ukiangalia sheria iliyopo sasa hivi ilikuwa inampa mamlaka makubwa sana Gavana. Kila mahali ilikuwa inasema *The Governor shall* na kadhalika. Lakini Muswada huu sasa tunatoa mamlaka kwa Gavana na kuipa

Bodi ya Benki Kuu. Mimi nafikiri upande wa maamuzi ni Muswada ambao umekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizingatia vile vile ni kwamba majukumu ya Benki Kuu sote tumeshaelezwa hapa na semina iliweza kuainisha vizuri zaidi na hata kwenye Muswada huu yameweza kuainishwa vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kuongezea ni kwamba muda huu ni muafaka kwa Benki Kuu sasa kufanya majukumu yake vema zaidi kwa maana ya kwamba sasa tunawapa nafasi. Kwanza ukiangalia ni kwamba Gavana atakuwa hafanyi maamuzi peke yake, tunamwekea *Deputy Governors* watatu hii inatoa nafasi kubwa sana kwa kufanya maamuzi. Benki hii inashughulika na mambo ya msingi katika kufanya maamuzi. Sasa unapogawanya madaraka inasaidia sana kufikia kwenye muafaka mzuri wa kufanya maamuzi sahihi kwa maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kumekuwa na wasiwasi kwa watu kwamba kwa nini Benki tunaipa uhuru zaidi, mimi sidhani kama tunaipa uhuru zaidi tunawabana zaidi sasa hivi kwa sababu Muswada huu unaelekeza kwamba kuna *a lot of accountability* na lazima sasa maamuzi yasifanywe na mtu mmoja zaidi yafanywe na timu ya wajumbe wa bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na haya katika Muswada huu kuna mambo ya kujaribu kuyaangalia. Kwa mfano ukiangalia katika Muswada huu bado hatujajielekeza zaidi kwa masuala ya riba na namna ya kuwaza ku- *control excess liquidity* kwenye *market.* Sasa hivi tunaambiwa kwamba Mabenki mengi sana yana fedha nyingi na watu hawana nafasi ya kuzipata fedha hizo. Akienda mkulima na mtu wa kawaida anaambiwa yeye hakopesheki. Sasa hili suala nadhani Benki Kuu watusaidie ili kiwe ni chombo ambacho kitasaidia zaidi wananchi kuweza kukopesheka na kuweza ku-*access* fedha kwenye haya Mabenki. Haina faida kuwa na fedha nyingi sana kwenye soko na kwenye Mabenki yetu lakini bado wananchi hawakopesheki. *(Makofi)*

Pili, suala la riba ni kubwa sana. Sasa hii bado haitoi *incentive* kwa mwananchi kuweza kukopa fedha Benki matokeo yake akikopa anacholipa ni kitu kikubwa zaidi. Sasa yote inakuwa *disincentive* kwa mtu kwenda kukopa fedha Benki. Lakini utakuta Mtanzania akipata hela yake ataanza kujenga nyumba kidogo kidogo mpaka atamaliza kwa *cash money* siyo kwa kukopa. Mambo ya *mortgage finance* lazima Benki itusaidie wananchi waweze kupata *mortgage finance* na waweze kupata fedha kuweza kuendeleza kujenga nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgao wa gawio una utata. Upande wa Zanzibar wanasema hawapati vizuri, upande wa Bara na sisi tunasema hatupati vizuri, kila mmoja analalamika kwa nafasi yake. Lakini ukiangalia huu mgao mzima wa gawio unategemeana na *ratio* iliyopo. Kitu ambacho Benki Kuu nadhani hawakufanya toka mapema na ningeomba iwe changamoto taarifa za kutoa gawio zitolewe mara kwa mara kwa wananchi ili waweze kufahamu kwamba katika mwaka huu Serikali ya Muungano imepata kiasi gani na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata kiasi gani. Ukiangalia

wenzangu kutoka Zanzibar wamekuwa wakizungumzia sana suala la kwamba gawio ni dogo. Lakini ukiangalia na *volume of transaction* zinazofanyika na *profit* inayopatikana ndiyo ambayo inaweza ikatoa *ratio* kwa ajili ya kutoa gawio hili.

Sasa ni vema ile *formula* ya kuweza kuwa na gawio hili, iweze kuwekwa sawia na wazi zaidi. Misingi ya kupata ile *formula* ieleweke ili kila upande usinung'unike. Kwa kweli unakuta kwamba upande mmoja unasema pengine unanyanyaswa au unanyonywa. Lakini si kweli iwapo mambo haya yatakuwa yako wazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *plan of action* ya *second generation of finance sector reform.* Tumeelezwa hapa ipo na ni moja ya mkakati kwenye Benki Kuu katika kutekeleza. Lakini ni vema katika muda mfupi ujao waweze kutupa *action plan* na ikiwezekana Bunge liwe linaarifiwa baadhi ya mambo ambayo yanafanyika ili tuweze kujua kwamba hii imefikia wapi na sisi kama Kamati ya Fedha na Uchumi na Wabunge hapa Bungeni tuweze kufuatilia kwa karibu zaidi na tuweze kuwashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuongezea hapa ni suala la thamani ya fedha yetu. Ukiangalia kila siku shilingi inashuka thamani, uchumi unakua, *inflation* inapungua. Sasa zote hizi ni *macro economic indicators* ambazo tunazo na Benki Kuu basi watusaidie kwamba unaposema kwamba uchumi unakua uwe *reflected* katika kuongezeka kwa thamani ya shilingi yetu. Sasa hivi unakwenda mahali unakuta shilingi inaporomoko, kwenye *bureau de change* inaporomoko, lakini uchumi wetu umekuwa ukikua muda hadi muda. *Inflation rate* iweze kupungua. Naomba sana hili suala Benki Kuu watusaidie katika kulitatua na kuona kwamba jinsi gani tuweze ku-*support* uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongelea suala la Muswada wa Benki Kuu, lakini kuna haja sasa kuangalia vile vile suala la hizi *pension funds* kwa sababu Benki *is a lender of the last resort* na Benki Kuu inahusika na fedha zote za nchi hii. Lakini unakuta kwamba suala zima la *pension funds* hapa Tanzania halijakuwa na *regulator* na hakuna mahali ambapo Benki Kuu imejihusisha moja kwa moja. Kuna haja sasa ya kujaribu kuliangalia vizuri sana. *Pensions Funds* zingine zina-*perform* vizuri zingine hazi-*perform* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia bado kuna manung'uniko ya hapa na pale. Lakini yote haya tunaomba kuwe na namna ambayo Benki Kuu waweze kuangalia kwa karibu sana. Hii ni fedha ya wananchi wale *pensioners.* Lakini vile vile hizi *pension funds* zina- *invest* hizi fedha ambayo ni vema Benki Kuu wasaidie kufanya *tracking* ili kwa maslahi ya wananchi na Watanzania wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa vile ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, sina haja ya kurudia ambayo yameshazungumzwa kwenye Kamati kwa sababu tumeyazungumza kwa pamoja na nayaafiki yote na nasema kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada ulioko mbele yetu.

Kwanza kabisa napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kuipongeza Serikali hususan Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Gavana na watendaji wote kuweza kuandaa sheria itakayowezesha Benki Kuu kuendeshwa katika viwango vinavyozingatia mifumo ya Kimataifa na hivyo kutuweka katika mazingira ya kushirikiana na wenzetu katika ushindani na kujenga uchumi kwa kasi inayostahili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nianze kwa kusema naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Aidha, nawapongeza Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri waliyofanya. Hii iendane kwa kuipongeza Serikali kwa kuwa sikivu na kushiriki katika mashauriano ambayo tumeyashuhudia kabla Muswada huu haujafika katika Bunge hili. Wabunge, tumepewa hata fursa ya kuwasikiliza wataalam walioshiriki katika mapendekezo ya Muswada. Jambo la kuvutia zaidi ni mabadiliko ambayo yamewasilishwa pamoja na Muswada wenyewe katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Huu ni ushahidi tosha kwamba wamekiri, nina maana Serikali imekubali mapendekezo ambayo kwa kweli yanaboresha Muswada wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimevutiwa pia jinsi upande wa Zanzibar ulivyoshirikishwa na Kambi ya Upinzani wameondoka wamefurahi kweli. Lakini kila mmoja anafurahi kwa sababu sote tuna maslahi katika Muungano. *(Makofi)*

Mimi nianze na hii kifungu cha 5 (1) marekebisho yaliyoongezwa yamenifurahisha sana kwa sababu katika shughuli za kibenki mambo ya msingi yaliyokuwa ndiyo yanahoji fikra zetu sisi Wabunge kwa niaba ya wananchi yamekubalika kuwemo. Kwamba Benki Kuu ijishughulishe na mambo ya mikopo kwa ajili ya watu kujiendeleza katika nyanja za kujenga nyumba na maendeleo kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kilimo. Kwa sababu sasa *mortgage financing* inakubalika, *development financing* inakubalika, *leasing financing* pia. Tutaweza kuwataka Benki Kuu kadri mambo yanavyowanyookea kifedha kujishirikisha katika mambo haya ya msingi na hivyo kusukuma maendeleo katika ngazi za Vijijini ambapo wananchi wengi ndiko wanakokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni hili la wajibu wa Benki kutengeneza na kutoa sarafu au noti. *The duty to issue currency.* Benki Kuu wana wajibu wa kutengeneza sarafu na noti. Lakini hivi karibuni kumetokea mvutano ambao hausaidii katika kuboresha huduma ya kifedha katika Mabenki. Katika Mikoa ya mbali na hata ya kati ya nchi yetu, mimi nisemee Mkoa wa Kagera sisi tayari tuna tatizo, *coins* hazifiki kwa jinsi inavyotakiwa, noti haziji kwa jinsi inavyotakiwa. Ukienda *CRDB* au *NBC* kutafuta noti ya shilingi 500, shilingi 2000, zinakuwa chafu haijapata kutokea. *Coins* za shilingi 100 hazisomeki! Unakuwa kama unampa mtu chuma tu. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa hii inatokana na mvutano wa Benki Kuu na hizi Benki ambazo hazijapata nguvu kama ya Benki yenyewe. Sasa baba anapobishana na mtoto anayemlea kwa

kubeba mzigo kuna walakini katika uwajibikaji. Nimesikia maelezo juzi kwenye semina Gavana anasema kwa nia njema kabisa kuwa tatizo linatokana na kukwepa jukumu la gharama ya kubeba *coins* na *notes* yaani sarafu na hizi noti.

Sasa mimi nashauri hivi kwa sasa Gavana, Benki Kuu *(BOT)* na Waziri wa Fedha washauriane waone *BOT* ibebe mzigo huu. Benki Kuu wana fedha waweke kwenye ndege noti watuletee mpya na sisi tushike waachane kuvutana na *CRDB.* Kwanza na ujambazi huu uliovyokithiri wa ni hatari. Hawa Benki ndogo hawana uwezo wa kubeba hizo fedha. Kwa hiyo, mimi nasisitiza *seriously* hii imetuathiri sana vijijini. Noti ni chafu, *coins* hazisomeki, kumbe ziko, Gavana anasema zimejazana kweli hahitaji kutengeneza mpya. Zipo ila shida ni ubebaji! Mheshimiwa Gavana, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu umenisikia kwenye hili ni jambo zito naomba mlifuatilie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, uhuru wa Benki Kuu ambao waliutaka Benki Kuu, wameupata na naamini wameridhika pamoja na marekebisho ambayo yamewekwa humu ya nia njema tu kwa sababu siyo uhuru wa kuifanya Benki Kuu iwe huru zaidi hata na Bunge, iwe huru dhidi hata ya Waziri wa Fedha, pamoja na kwamba Gavana anateuliwa na Rais. Sasa hiyo ingeshangaza sana. Mimi nimevutiwa na haya marekebisho mliyoyaweka kifungu cha 50(2), Gavana siyo amjulishe Waziri wa Fedha kuhusu sera ya *exchange rate,* washauriane, waafikiane na Waziri lazima atakuwa ameshauriana na wataalam wazito wa mambo ya fedha. Wataweza kujua mabadiliko yanayopendekezwa na pande zote yanazingatia maslahi au uhai wa nchi. Kwa hiyo, mimi nimevutiwa na hii. *They must consult,* siyo kumu-*inform* Waziri wa Fedha. Hiyo imezingatiwa, hivyo Serikali ni sikivu, mimi naendelea kuwapongeza Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20 (6) baada ya marekebisho, mwanzoni nilikuwa nashangaa nilipoisoma *bill.* Hawa Benki Kuu ukaguzi watafanyaje wakati malengo ya Muswada wenyewe ni kuweka uwazi, uwajibikaji na hivyo kuwa katika mfumo wa kuweza kufikia viwango vya Kimataifa katika kusimamia Mabenki ambayo yanakuwa kwa kasi sasa hivi. Halafu inapofika kwenye ukaguzi wanazungumza namna ambayo ilikuwa haieleweki sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nimevutiwa na Kifungu cha 20(6) mpya iliyoongezwa. Wajibu wa Benki Kuu kukaguliwa na *Controller and Auditor General* (Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali) na vile vile kuheshimu sheria yetu ya fedha za umma *(Public Finance Act). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi mmefanya kazi nzuri sana na ahsante sana. Hiyo inaonyesha dhahiri na Serikali kukubali Benki Kuu hawakuwa na nia ya kukwepa. Wanataka tu waweke mambo kwa *speed* ili wayasimamie kwa utaratibu waliokuwa wamependekeza.

Sasa kwa kuweka viwango vya Kimataifa na vya ndani wamenifurahisha sana, kwa sababu na sisi tuna *legal framework* ya kusimamia mambo haya kwa uwazi na uwajibikaji kwa kuzingatia utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la muda wa uzoefu wa nani anafaa kuwa Gavana wa Benki Kuu. Sijui kwa nini Serikali mnakuwa wagumu, imeelezwa sana kwenye semina sasa hivi tuko kwenye kikao rasmi. Walionitangulia nimesikia wanasema miaka 15 ya uzoefu ni mingi. Kwa kweli ni mingi mno. Kwanza miaka 10 ya uzoefu hata na yenyewe ni mingi. Hivi kuwa Gavana ni kitu cha ajabu sana? Miaka 15 ya uzoefu mtu anatafuta sifa, Mwanasheria vile vile kwa mapendekezo ya Muswada huu anaweza wakati miaka mitano unakuwa Jaji! Yaani uzoefu miaka 15 ndiyo uwe Gavana, *why? (Kicheko/Makofi)*

Naomba Serikali mtuelewe tafadhali. Sisi hatuna nia ya kuvuruga Miswada yenu. Nimemwuliza jirani yangu hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi hili hamkuliona? Akasema hili hatukulipata sawasawa. Ni uwazi na ukweli. Sasa nawaomba tafadhali, teremsha angalau iwe miaka hii10, inaweza kuwa *compromise* kwa sababu gani, wastani wa uhai wa Mtanzania kuishi watu wanavyotueleza kwa sababu ya UKIMWI umeshuka mpaka miaka 50, *yes* na wengine wanashusha wanasema ni miaka 45 yaani *average life expectance* ya Mtanzania ni miaka arobaini na tano. Ni mambo ya kutisha.Halafu tunasema mtu miaka 15 ya uzoefu kuwa Gavana yaani watu watakuwa wamekufa, wamekwisha, kuja kupata sifa ya kuwa Gavana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wenye sifa za Gavana mtawatoa nje hawa watu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uliangalie. Hiyo ni kengele ya kwanza, naendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Eneo lingine ambalo limenishangaza sana na naomba Serikali katika kujibu, Mheshimiwa Waziri anisaidie. Hivi katika kifungu cha 52 kifungu kidogo cha (1) (a), tumeanza, mnatuomba sisi Bunge tuidhinishe kwamba mojawapo ya shughuli za Benki Kuu muweze hata kuagiza dhahabu kutoka nje ya nchi! Kwa nini? Mimi naweza nikaelewa baadaye sana tukishachimba hii dhahabu iliyopo mpaka tukasema inakaribia kwisha ardhini, ndiyo tutasema Benki Kuu jiandae tunaweza kuhitaji kuagiza nje. Sana sana mimi ningependa Benki Kuu wawekeze kwenye kuchimba dhahabu ya ndani,siyo kwenda kuziagiza nje. Sasa tutakwenda ku-*import* za wapi tena. Hiyo mimi sitaki kusema siwaamini *BOT,* nataka kusema hivi kwa nini Bunge tukae mwaka 2006 kuidhinisha kuagiza nje dhahabu hatujazimaliza nchini wakati mirabaha bado inatupa kasheshe. Mirahaba sijui Mrabaha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tafadhali sana mlifikirie hilo, Serikali tunaomba, siombi jambo lingine, kifungu cha 52(1) futa hiyo *import* ibaki *export, buy, sale, hold or otherwise deal in gold.* Baadaye mtakuja mkitaka, mbona huu Muswada ni baada ya miaka 10 ndio mkaja kuomba sheria mpya? Mkizitaka kutoka nje *(mport)* mje tena hapa. Msije mkaanza kuzi-*import* dhahabu toka nje wakati si busara ku-*import. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hii imeungwa mkono. Ahsante sana. Nadhani Serikali itaipa uzito, maana yake wanaotafsiri tulikusudia nini Wanasheria, watasoma *Hansard* na makofi haya yatakuwa kwenye *Hansard. (Kicheko)*

Mimi napenda kukushukuru ili nikae chini Mheshimiwa Naibu Spika kwamba kwa kweli Bunge letu linapeleka ujumbe mzito kwa wawekezaji katika Sekta ya Fedha kwamba kwa *speed* ya ukali tumeruhusu Serikali iendelee na sheria hii mpya, kwa moyo mkunjufu tena *by consensus* kwa sababu hata Wapinzani wameunga mkono. Kwa hiyo, hakuna Benki itakayofunga *Branch* yake. Zote zitaendeleza biashara hapa hapa na mimi nawaunga mkono muendelee ili kusudi ile benki iliyofungwa kwenye Tarafa ya Nshamba labda *inshallah* mtaifungua tena. Walifunga eti hatukopi, tunaweka tu. Sasa tuko kwenye vi-*saccos.*Sasa endelea kwa kasi ili kusudi Benki zije zikose nafasi Dar es Salaam, zikose nafasi Arusha, zikose nafasi Mwanza, zifike kwenye Tarafa ya Nshamba na Muleba Kusini yote ili na sisi tuache kuweka pesa zetu kwenye vichungu chungu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki haziji huko, eti wananchi vijijini wanaweka, hawakopi. Mimi hapo ndiyo nilijifunza kumbe benki ni *complicated,* kumbe kazi yake siyo kuweka tu, lazima ukope. Usipokopa wanafunga hawa watu. *They don't need your money if you don't borrow.* Sasa sisi tunajitahidi kujifunza kukopa, kwa hiyo, ninyi jazeni mabenki waje wengine wengi, mkijaa huko mtafika kule pembezoni na sisi tutakopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR SHEHA MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi miongoni mwa wasemaji wa mwanzo kuchangia Muswada huu. Vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Gavana na timu yao iliyowasaidia kuandaa Muswada huu na leo kufika hapa Bungeni kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafasi hii kidogo kuelezea historia ya Benki Kuu ya Tanzania na haswa hizi sheria zake zote ambazo zinabadilishwa na hasa hii ya tatu ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa kwa sheria ya mwanzo ya mwaka 1965. Sheria hii ya mwaka 1965 ilifanya kazi kwa miaka 30 bila kutumika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kule Zanzibar. Sababu kubwa ya kutumika sheria hii Zanzibar ni kwa sababu hapakuwa na maelewano baina ya pande zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wakati ule. Lakini kwa busara za viongozi wetu tulianza kujadili masuala ya muafaka kuanzia mwaka 1992 pale Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Awamu ya Pili na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Tano zilipoanza kuanzisha mazungumzo ya muafaka na hii sheria ya Benki Kuu ni mojawapo ya suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wakati ule tulifikia mahali kwamba tukasema jamani huu ugomvi uishe na nakumbuka kabisa mwaka 1993, Desemba katika kikao cha muafaka ambacho kiliongozwa na Waziri Mkuu, Mzee John Malecela wakati ule tukakubaliana kwamba sasa bwana ugomvi umekwisha, basi tuwe na Benki Kuu moja, sarafu moja ya fedha, Mamlaka moja ya Usimamizi wa Fedha na Mamlaka moja ya Usimamizi wa Mabenki na ndiyo sheria hii ya mwaka 1995 ya Benki Kuu ambayo ipo mpaka sasa hivi ilivyotungwa na kwa maana hiyo, Sheria tunayoifuta sasa hivi ni sheria ya Muafaka. *(Makofi)*

Sasa basi nini tofauti baina ya sheria hii inayofutwa na hii tunayoitaka kuiweka sasa hivi. Tofauti hasa iko katika maeneo mawili makubwa. Ni kweli kabisa Benki Kuu na mambo matatu makubwa, kwanza *autonomy* au *independence* kama ilivyokuwa katika sheria hii ya sasa hivi. Pili, suala la *tax exemption* ambayo Benki Kuu bado ina-*enjoy* na tatu suala zima la *concentration* ya shughuli zake kwenye *Monetary Policy.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya sasa hivi na Sheria hii mpya ni kwamba Sheria hii mpya bila shaka inatungwa kulingana na wakati ulivyobadilika na kwa kweli mimi nakubali kabisa kwamba Benki Kuu kwa miaka 10 iliyopita imefanya vizuri na imefanya vizuri kwa sababu ya haya mambo matatu niliyosema. Kwanza *independence* iliyokuwepo na pili *tax exemption situation* ambayo Benki hii ina-*enjoy* na tatu suala zima la ku-*concentrate* kasi mpya hii ya kushughulikia *Monetary Policy. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya shughuli zake Benki Kuu kuna jambo moja ambalo kidogo ningependa nilizungumzie. Suala zima la mtiririko na mageuzi na tofauti kwenye uongozi wa Benki Kuu. Kwa Sheria ya sasa hivi ambayo tunaifuta, Bodi ya Wakurugenzi wa Benki Kuu ilikuwa na Wajumbe 10, wote walikuwa na *power* ya *voting rights.* Na hii ya sasa hivi vile vile ina Wajumbe 10 lakini tofauti yake ni kwamba ile ya zamani au hii tunayoifuta ilikuwa na Wajumbe 6 ambayo ni *non-executive.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wajumbe wawili, *Governor, Deputy Governor* ambao ni *Executives* na Wajumbe wawili *Ex-Officials.* Sasa hii ya sasa hivi ina Wajumbe nane ambao wamewekwa sawa sawa. Wanne ni *non-Executives* na wanne ni *Executives* kwa maana ya Gavana na ma-*Deputy Governor* watatu pamoja na wale wawili wa *Ex-Official* ambao hawawezi ku-*vote.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii bila shaka ni tofauti ambayo ni muhimu kuwawezesha Benki Kuu kufanya vizuri zaidi kuliko kipindi kilichopita. Wasiwasi wangu ni kwenye sehemu mbili. Katika kipindi hiki cha miaka 12 iliyopita tokea kukubaliana juu ya masuala haya ya gawio.

Kwanza nataka niseme suala la gawio halikuja *automatic.* Limekuja kwa muafaka na maelewano. Lakini bahati mbaya toka kuelewana mwaka 1994 kama nilivyoeleza, kikao kile cha Desemba 23, Ikulu, baada ya muda uliofuatia miaka 10 hapakufanywa chochote ili kuendeleza muafaka pamoja na suala hili la Benki Kuu. Sasa hii maana yake nini. Maana yake ni kwamba bila shaka tunaheshimu Sheria. Lakini kitu cha kushangaza ni kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha ilioundwa mwaka 1996 mpaka leo

mwaka 2006 ni miaka 10. Sheria hii ililetwa Bungeni kwa nia njema tu ya kusaidia kutatua matatizo na kero za Muungano.

Lakini bahati mbaya mpaka leo haijaanza kazi. Sasa hili lalamiko la gawio nadhani kisingizio chake ni kwa sababu ya kutofanya kazi hii Tume ya Fedha ya Pamoja.Tunachoomba ni kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa labda kuja ku-*wind up* kwenye Muswada huu atuhakikishie angalau kwenye Bajeti inayokuja basi suala hili kutakuwa na mwelekeo au kauli ya Hazina nini juu ya jukumu au walipofikia Tume ya Pamoja ya Fedha na hasa kutatua suala hili la gawio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu ni juzi tu tumepewa takwimu ya Benki Kuu na nasema haya vile vile kwamba mimi nilishiriki katika muafaka ule wa mwanzo na nakumbuka vizuri tulipoanza na utekelezaji wa gawio kwa kweli ilikuwa faida ya Benki Kuu inaanzia *between* milioni 12, 14 na kuendelea, ile faida ambayo inapelekwa Mfuko Mkuu wa Hazina. Lakini mwaka jana mahesabu ya Benki Kuu yaliyoanzia Juni gawio la Serikali zote mbili ni bilioni 1.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kwamba tumeanza vizuri tulipokubaliana muafaka.Lakini sasa tunaelekea kupuuza muafaka ule. Ninachosema ni kwamba kwa *spirit* ile ile ya makubaliano basi hii sheria mpya ichukue na izingatie masuala haya na hasa *technically* nipozungumzia nakwenda kwenye ukurasa wa 42 wa hii sheria ambayo tunataka kuibadilisha.

Ukurasa wa 42, kifungu cha 23 hapa inazungumzia kwamba Benki Kuu katika kufanya shughuli zake haitoingiliwa na Sheria ya Makampuni kwa vyovyote vile. Lakini Sheria sasa hivi inazungumza kwamba haitaingiliwa na Sheria ya Makampuni isipokuwa kwa Sheria nyingine itakayotungwa na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano na saa nne zilizopita hapa tumekubaliana pamoja na Mheshimiwa Waziri yule pale kwamba kifungu hiki cha 23 kiongezwe maneno *accept persuant to the Act of Parliament* na Waziri ametukubalia. Lakini katika *schedule of amendment* hamna suala hili.

Kwa hiyo, hapa nitakuja juu sana mimi na wenzangu kwa suala hili. Tunataka sahihisho hili liwekwe.Haiwezekani Benki Kuu pamoja na uhuru huu tuliowapa, nguvu zote tumewapa, hawawajibiki, hata kwa Bunge inakuwa haiwezekani. *(Makofi)*

Hili ni ombi langu la kwanza. La pili, ni ukurasa wa 38. Ukurasa wa 38, kifungu cha 18(1)(d) kifungu hiki kinasomeka kwamba *other special reserves or funds from time to time from appropriation of net profit.* Maana yake ni kwamba Benki Kuu au Bodi imepewa uwezo wa kufungua mifuko kama itakavyoona inafaa ambayo itatokana na fedha za mapato yake ya faida ghafi. Sasa hapa napo ndipo ninapotaka tuangalie vizuri sana juu ya kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika utaratibu huu wa kushuka gawio kila mwaka kifungu hiki kikiachwa kama kilivyo bila kuainisha mifuko ipi na maeneo yapi itafika wakati hakuna Serikali itapata gawio katika suala hili. Kwa hiyo, hili naomba nalo vile vile ulizingatie na namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja

kujibu atuhakikishie hili kwa sababu hii hofu siyo mimi peke yangu, hofu pia ni kwa wasemaji wengine vile vile wamezungumza kwamba kila tukienda gawio linashuka. Sasa jamani kama mtoto umemzaa unampa uhuru basi hawezi hata kuruhusu baba naye akapata chochote aliyemzaa kwa maana ya wenye hisa Serikali hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba anapokuja Mheshimiwa Waziri wa Fedha na hili atusaidie kidogo ili tuwe na matumaini kwamba Bunge hili linapitisha Muswada huu lakini vile vile Serikali nayo inaishi. Siyo vizuri kuishi Benki Kuu peke yake. Lakini mwenye hisa akawa anasononeka au anaumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono Muswada huu na naomba sana haya niliyoyasema yazingatiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake, Katibu Mkuu na wote waliosaidia Muswada huu bila ya kuwasahau Wanakamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Muswada huu nauunga mkono mia kwa mia. Hakika umekuja kwa wakati muafaka na ninaamini ndiyo dunia ya kisasa, lazima twende na dunia, ndiyo inavyotuambia. Duniani kote Benki Kuu lazima iwe *independent. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yangu sasa kwamba kuna mambo ambayo pamoja na *all the independence* watakaokuwa nao, kuna mambo lazima wayazingatie katika shughuli za kila siku. Kazi yao kubwa ni kusimamia *Monetary Policy.* Lakini kazi yoyote ya *Central Bank* ni kuhakikisha wana-*maintain stability* ya *national currency* na *money supply.* Sasa ukiangalia *our national currency* haiko *stable* niwaombe sasa baada kwamba sasa wana *all this independence* hili nalo walisimamie kwa uhakika zaidi ili tuone faida ya hiyo *independence* tunayowapa leo.

Lakini pia kuna suala la *interest rate.* Wenzangu wameliongelea, niwaombe wenzangu wa *BOT* hili nalo waliangalie kwa umakini mkubwa. *Interest rates* zinatisha kidogo. Ni kubwa sana na ndiyo maana leo mabenki mengi yana pesa nyingi kwa sababu watu wanaacha kwenda kukopa sasa kwa sababu unapoanza kurudisha ni ngumu kweli kweli. Kwa hiyo, ningeomba suala hili la *interest rate* nalo walisimamie kwa umakini mkubwa. Jambo lingine ambalo mimi nimeliangalia sina tatizo na Magavana watatu, sina tatizo kabisa. Kwa sababu ukiangalia *functions* zao zinakidhi kuwa na Magavana watatu, ma-*Deputy Governors* watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kazi za *Deputy Governor* ni kusimamia mabenki, *bank supervision,* ni matarajio yangu sasa tusirudi kule nyuma. Sasa tusikie kesho kuna benki imeanguka wakati kuna *Deputy Governor* ambaye siku zote anaangalia *operation* za hizo Benki. *(Makofi)*

Lakini pia katika suala hili la ma-*Deputy Governors* Sheria inasema *Deputy Governor* mmoja atakuwa Mzanzibar. Mimi ningeomba, ninajua nitaonekana niko *gender bias,* ningependa kama inawezekana *one of the Deputy Governor* awe mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu tu ambazo zinafahamika, akinamama kwa kweli ni waaminifu zaidi jamani. Lakini pia katika hili la *Deputy Governors* na *Governor. Deputy Governors* watatu, pamoja na Gavana, wote ni *members* wa Bodi. Ukisoma sheria huku ndani, wanasema kukitokea suala la dharura waka-*convene,* watafanya maamuzi baadaye wataitaarifu Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaombe wasije wakakaa *as a management* wanafanya *decision as a management* baadaye unagundua hiyo *decision* ya Bodi wanajigeuza muda huo huo wanakaa kama Bodi. Ningependa wajitahidi sana *unless* ni *necessary* ndiyo wafanye maamuzi ambayo yangefanywa na Bodi. Lakini wajitahidi mara nyingi wale wa nje wawe wanakuwemo katika maamuzi ya Bodi, uaminifu utakuwa mkubwa zaidi. Kwa sababu tusipoangalia hapa tukipata Gavana ambaye yeye akasema mimi ndiyo Mwenyekiti, mimi ndiyo Gavana, matokeo yake anaweza kuwa kila *decision* anasema ni ya dharura hata ambayo si ya dharura wanafanya *decision* na ma-*Governors* wake wanakuja kuitaarifu Bodi baadaye. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba wajitahidi sana, *unless it is very necessary* wasifanye maamuzi ya Bodi wawe wanne kwa sababu sheria inawaruhusu waje kuwaambia wenzao baadaye. Wajitahidi sana ku-*make sure* mara nyingi sana wawa-*involve* wale watu wa nje. Kwa sababu tu moja, wale watu wa nje hawakuwemo kwenye mambo yao ya kila, shughuli zao za utendaji. Wanakuja na *new fresh thinking,* nayo ni muhimu kui-*observe* katika maamuzi ya Bodi. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo mimi kwangu naona ni la muhimu sana, watu wa *BOT* watusaidie, tunahitaji *stable economy, stable currency* na waweze ku-*manage inflation as well as inflation.* Ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yoyote. Lakini pia suala la *exchange rate. Exchange rate* unaweza ukai-*manage* na kuna *exchange rate* ambayo inakuwa *managed* na *market* na kuna ambazo zinakuwa *there at between.*

Kwa hiyo, zile ambazo unaweza uka-*manage* wajitahidi ku-*manage exchange rates* kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nasema *independence* ya benki ni muhimu sana ili waweze kufanya *credible monetary policy.* Ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Baada ya kusema hayo mimi kwa kweli niwashukuru. Nimshukuru Waziri wa Fedha kwa sababu Waziri wa Fedha kuamua kuleta Muswada huu kwa namna moja au nyingine amewapa nguvu kubwa sana watu wa benki wawe *independent,* waweze kufanya kazi yao vizuri. Siyo watu wengi wanaweza wakaikubali hiyo. Kwa *nature* ya binadamu ile *supremacy* Waziri wa Fedha mwingine angependa iendelee kuwepo. Lakini Waziri wa Fedha amekubali kwamba Benki yetu iwe *independence* na ni

matumaini yetu benki yetu hawatatumia vibaya hiyo *independence* ambayo leo wanapewa, iwe kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi ninaunga mkono hoja na huu wakati umefika na sisi twende kwenye *international standard.* Nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika na mimi kupata nafasi usiku huu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kuhusu Benki Kuu ya Tanzania.

Kabla sijaendelea, ningependa niseme neno moja kwa ruhusa ya Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa hatukuja hapa kujibu hoja. Lakini tunachangia hoja. Kutokana na kuzingatia *agenda* kama alivyozungumza msemaji aliyepita kuhusu kuchagua Magavana, niipongeze kwanza Serikali kwamba imeanza kumchagua Waziri wa Fedha mwanamke kabla haitakuwa kapu. Kwa hiyo, natumaini kwamba itakapofika huko itazingatiwa. Kwa hivyo, ndugu wajumbe wasiwe na wasi wasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwanza niseme kwamba naiunga mkono hoja hii maana yake nina kawaida ya kusahau sahau, nisije nikasahau nikaiacha. Lakini niseme tu kwamba binadamu tulivyoumbwa tumepewa siku tatu tukufu. Siku yetu ya kuzaliwa, siku ya kuoa au kuolewa na siku ya kufa. Lakini binadamu tulipofika hapa duniani, tukasema kwamba katika hayo tulete na fujo. Baada ya hizo furaha tulizopewa tukasema tutafute na fujo na fujo tulizozitafuta tukazitafuta fujo kwa watoto, mali yaani fedha na mke au mume.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko mbele ya Bunge hapa, tunajadili suala la sheria kuhusiana na fedha. Nafikiri madhumuni ni kujaribu kutafuta njia ya kupunguza fujo na ghasia kati yetu. Kwa hiyo, niipongeze sana Wizara ya Fedha kwa wakati huu kwa kuleta Muswada ili kuja kuzingatia hali halisi ya ulimwengu ulivyo pamoja na sisi binadamu na hulka zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambao waliuchambua Muswada huu wa Sheria pamoja na Serikali hasa kwa kuwaunganisha, sehemu ya pili ya Muungano yaani Zanzibar kwa ukamilifu. Hii ina maana wazi kwamba bado lengo ni lile lile kupunguza fujo na msukumano kati yetu. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali pamoja na Kamati na Wajumbe wote kwa hatua hii na hasa wale Wajumbe wa Zanzibar ambao walikuja wakachangia Muswada huu ambao na sisi utuwezesha kwa kiasi fulani kupunguza zile hoja za kuweza kuihoji Bunge zaidi ya kusema kwamba tunatafuta marekebisho madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kizuri hua hakikosi kasoro au marekebisho kwa wengine. Kwa hiyo, na mimi nataka niwe mmoja wa kusaidia kutoa mawazo kuhusiana na Muswada huu wa Sheria. Muswada umekuja, umezungumza vizuri kuhusiana na suala zima la kuchagua ma-Gavana na *Deputy Governors* pamoja na ma-*Directors* ambao

watahusika na suala hili. Lakini tukizingatia maelezo ambayo yametolewa na wataalam wetu wa fedha, wasemaji waliopita ilionyesha wazi kwamba kulikuwa na mvutano na kasoro fulani fulani hasa zinazozingatia masuala ya mgao.

Kwa hiyo, ningesisitiza na kuishauri sana Serikali ikakaa na ikazingatia ipasavyo huu mgao wa asilimia 4.5 unaokwenda kwa Serikali ya Zanzibar kutokana na faida hii ikawa ni kielelezo cha kupunguza fujo na ghasia na kuleta muafaka unaofaa katika Serikali zetu hizi zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na katika suala hili vile vile tuzingatie kwamba hivi sasa Benki Kuu, nimepita Dar es Salaam pale mbele tu ya ofisi yetu ya Bunge, ofisi ndogo.

Kuna majengo makubwa sana ambayo haijapata kutokea na majengo haya yote ni kwa sababu ya kuichunga na kuiendeleza fedha. Itahitaji wataalam na kwa mara ya kwanza katika historia kule Zanzibar tumepata ofisi. Naweza nikasema kwamba itakuwa pengine ikimalizika, jumba la ghorofa nane la aina yake itakuwa ndiyo ofisi pekee yenye hadhi kama hiyo ya Benki Kuu.

Sasa ikiwa kama hii ndiyo hali, tegemeo langu kubwa ni kwamba kama tulivyokuwa na uwiano mzuri wa jinsi ya kuendeleza fedha tutakuwa na uwiano mzuri katika kuchagua na kuwaweka magavana pamoja na Wajumbe wa Bodi katika hali sawa ya kuzingatia Zanzibar na kuzingatia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vile vile.

Sasa kama hii ndio hali halisi na mabenki mengi sasa hivi yanakuja, mabenki yako ya nchi za nje, mabenki yetu ya Zanzibar na benki za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(NBC)* zinafungua matawi katika sehemu mbalimbali.

Kwa hiyo, ikiwa kama sasa tumefikia kiwango kwamba tumepata ofisi ya Benki Kuu na natumai tutapata watendaji wa Benki Kuu sio wazee wa kwamba bado miaka miwili kufariki kama ilivyozungumzwa, lakini ni vijana waliokuwa wakakamavu, natumai kwamba tutaweza tukafikia hali nzuri na kuona kwamba fedha zetu zinatunzika vizuri na amani yetu ya utulivu inaendelea kwa hali inayoridhisha katika mpango huu wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Napendelea sana kwamba ari hizi, nguvu hizi na kasi hizi zielekee katika kudumisha Muungano wetu katika kudumisha usalama na amani katika nchi yetu hii ya Tanzania

Sasa faida ya fedha, ni kuwasaidia wananchi waliokuwa matajiri na waliokuwa maskini. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba mabenki yetu haya ambayo yanatoa mikopo ambayo kwa kiasi fulani Zanzibar hayafiki sana na najua nafikiri ni benki chache sana zinazotoa mikopo kwa Zanzibar, lakini riba imekuwa kubwa mno na haizingatii kwamba leo mimi kama mwananchi nikiweka hela yangu pale napewa faida pengine *three* au *four percent,* lakini ninapokwenda kukopa nalipa riba ya 20% jamani hizi hesabu za kibenki mie sio mtaalam lakini kwa nini zisizingatie hali hii halisi ilivyo kwamba ili kuwapa na nafasi walau na sisi tuliokuwa katika hali ya chini tuweze na sisi kujiendeleza na kujiondolea umaskini kwa kutumia mikopo inayotokana na mabenki yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo zuri kuona kwamba leo kama sisi Waheshimiwa Wabunge tumepewa miaka mitano lakini unamkuta mtu anakopa huko miaka miwili au anachukua riba dhamana inakuwa nyingine, unajua kuna baadhi ya nchi ambazo dhamana kama unayo nyumba au ule ule mkopo wako ndio wanachukulia dhamana, kwa nini na sisi hapa benki zetu Benki Kuu isifuate taratibu hizo za kuona kwamba walau watu wa hali ya chini na wao wananufaika kwa kuwa na mikopo ya muda mrefu na iliyokuwa na riba za nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nadhani na mimi nimesikika, lakini nisisitize tu kwamba shughuli zetu hizi za kibenki ni lazima ziende kulingana na hali yetu ya uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia juu ya Muswada huu.

Kwanza kama walivyosema Waheshimiwa wenzangu wengine na mimi naunga mkono Muswada huu upite. Ninayo mambo machache ambayo ningependa kuyasema kuhusu Muswada wenyewe lakini nilikuwa nataka kusema mambo mawili ya utangulizi, kwanza kabisa ningependa kuwapongeza Gavana wa Benki Kuu na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya hivi mpaka sasa. Katika kipindi cha miaka kumi walitoa kitabu hiki ambao Waheshimiwa Wabunge wote tumegawiwa, ukisoma utaona kazi na majukumu walizotekeleza kwa kweli wanastahili pongezi sana hasa tukizingatia kwamba nchi kama Tanzania, Benki Kuu yetu inaongozwa na Watanzania watupu hakuna wageni ndani ya benki yetu. *(Makofi)*

Baadhi yetu tuliopata nafasi ya kufanya kazi karibu nao hasa kwenye Kamati ya Fedha ambayo nilikuwa zamani tulizungumza mambo mengi sana ya kuelekeza Benki hii hasa ya usimamizi wa sekta hii ya fedha na tukawa tunashauri waanze kujitoa kidogo kidogo kutoka tabia ya kawaida tu maana watu wengi ukisema Benki Kuu wanafikiria tu kwamba kazi yao ni kuchapisha noti lakini kumbe wanakazi zaidi na mimi nafurahi sasa kutokana na kukua huku, sasa benki yetu na Serikali yetu wametuletea Muswada huu ambao tunaujadili na nataka pia nimpongeze Waziri wa Fedha, kwamba alivyoelezea jambo hili utafikiri alishakuwa Waziri wa Fedha kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Lakini nataka pia niseme jambo lingine kwamba mambo haya tunayozungumza hasa sisi wanasiasa, lazima yalenge kusaidia maendeleo na kutekeleza Ilani yetu ya uchaguzi ya mwaka 2005/2010, ndio labda uwe msingi wa mambo haya na nafurahi kusema kwamba awamu ya nne ya Serikali yetu kwa namna walivyoanza kila mtu wa Tanzania tumeanza kupata matumaini makubwa sana kwamba watatekeleza Ilani ya uchaguzi kama tulivyoipanga. Lakini nafurahi vile vile niseme mbele yenu Waheshimiwa mimi nimefurahia sana hekima ya Rais wetu wa awamu ya nne, ndugu yetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sababu tulipokuwa nje kwanza nataka niseme rasmi kwamba mimi nimepata bahati ya kutoka naye nje ya nchi, kweli kila mara tulikwenda ni Rais wa nchi

tuliona heshima kubwa sana, hatukutembea na mtu anayefanana kuwa Rais tulitembea na mtu ambaye ni Rais wa nchi na heshima ni kubwa hata viongozi waliomtangulia tuliona wanavyomheshimu na hotuba zake zote zimejenga kweli heshima ya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba tumuombee mwenyezi mungu amjalie afya njema. *(Makofi)*

Lakini jambo kubwa nataka kulisema hapa mkiona humu kwenye taarifa hii wanasema Benki Kuu wanasema kuwa mwaka 1995 wakati wa awamu ya tatu ilipoingia, kulikuwa *reserve* yetu ya fedha za kigeni ilikuwa dola milioni 269 na mwaka jana tulipofanya uchaguzi wetu na taarifa hii ni ya mwaka 2004 akiba ya fedha ya kigeni tuliokuwa nayo baada ya miaka kumi imepanda kutoka milioni 267 na kufikia bilioni 2.3 haya ni mafanikio makubwa sana.

Sasa tulipokuwa na Rais wetu alikuwa akizungumza na Watanzania, anasema hivi nataka niwafahamisheni kwamba hatutayumba, nina nguvu kwa sababu Rais aliyenitangulia ameacha msingi mzuri wa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanataka tutambue hekima ya Rais huyu ambaye amechukua madaraka kwa Rais mwenzake wa Serikali ya chama chake na anatambua na kueleza mambo kama haya na anasema wanae Tanzania mlioingia mjivune, kwamba uchumi wetu sasa ni asilimia 6.7 na mimi naamini ataupandisha zaidi, anasema sifa inayotakiwa ipatikane sio watu waseme tulikupa urais, lazima waseme ulitukuta hapa umetufikisha hapa. Sasa hiyo ni tabia ya kiongozi mzuri anayetambua mwenzake aliyetangulia, kwa hiyo, mimi nataka kwa sababu nawashangaa baadhi magazeti wakiandika utafikiri Serikali ya awamu ya tatu hawakufanya hata kitu hata kimoja. Sasa ni aibu wanajiabisha bure, kwa sababu Rais mwenyewe, kwanza Rais huyu ni wa CCM na anatekeleza sera za CCM ambazo mafanikio yake ya mwaka 2000/2005 zimetuwezesha watu kutuamini kuendelea.

Kwa hiyo, nataka mimi niseme watu wa magazeti oneni aibu kuandika, kutukana mambo ambayo hamjui, jifunzeni hivyo hata taarifa hizi magazeti yetu hawasomi. Sifa ya nchi yetu ni kubwa sana, tumetoka na sifa nzuri, matumaini makubwa kwa sifa nzuri na mimi nimeelewa *philosophy* ya Rais wetu, anasema unapochukua nchi ambayo mwenzako katangulia kafanya vizuri, lazima uende na kasi mpya na nguvu mpya ndio tafsiri yake ni kutoka pale, kwa hiyo, nataka niseme haya kisiasa kwa sababu watu wengine ni kama hawaelewi tulikotoka na tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hayo ningependa niseme mambo matatu, la kwanza, nchi za wenzetu zenye mafuata, kwa mfano wanajivunia mafuta na wanasema mimi nipo hata kupata nafasi ya Malaysia na nilipata bahati ya kuzungumza na Waziri Mkuu wa Malaysia, Martin Mohamed ametoka na sifa ya juu sana kuongoza nchi vizuri aliniambia akasema Mheshimiwa maana nilikwenda kutembelea michikichi nikiwa *Regional Commissioner* wa Kigoma kwa sababu tulikuwa na programu ya kulima michikichi, wakanitembeza, akaniambia mbegu hii ya michikichi mimi nilianza kuitoa Ivory, Kusini ya Nigeria. Nchi niliyokwenda wakati ule Malaysia kwa zao la michikichi peke yake mafuta yanayotokana na michikichi Malaysia walikuwa wanaingiaza, dola za Kimarekani 2.9 bilioni kwa mafuta ya mawese peke yake.

Sasa nilipomuuliza anasemaje, anasema bora mtakaa *it is very simple* mtu kuelewa, nasema ni rahisi kuelewa. Mimi nasema nina mafuta kwa hiyo mafuta sio *renewable resource* yatakwisha, mimi kila shilingi ninayopata natumbukiza kwenye kilimo na *number one* ni mchikichi. Sasa sisi tumejaliwa, nafikiria baada ya miaka matano, kumi ijayo inawezekana sisi Tanzania tukawa wa pili au wa tatu kwa kuchimba dhahabu, sasa lazima tujiulize swali na Benki Kuu mtusaidie kuielekeza Serikali. Hivi dhahabu tunayopata sasa imejenga barabara kilometa ngapi? Na imetuongezea mbolea kiasi gani, za kuweza kuongeza kilimo cha kahawa na chai na pamba? Maana faida moja ya kuwa dhahabu ni kusaidia kuendeleza sekta zingine kama vile kilimo na ujenzi wa miundombinu barabara sasa kitu kimoja niseme lami hii kilometa 100 unayoiona hii imetokana na dhahabu yetu, kwa vyovyote vile baada ya miaka kadhaa dhahabu yatabakia mashimo tu.

Sasa lazima tuwe na jibu maana *reserve* zimeongezeka na katika *reserve* kuongezeka, moja kilichoongeza *reserve* kwa vyovyote vile ni dhahabu na wote tunaona, sasa mimi ninachotaka kusema *challenge* hii kwa Benki Kuu na Serikali yetu kwamba vitu hivi vinavyotupa pesa sasa lazima tutazame zitatumikaje kutupa uwezo wa ziada. Kwa mfano, tuna fedha za kigeni sasa hizi fedha za kigeni kwa sasa hivi tumefungua mlango hakuna vibali vya kuagiza vitu kutoka nje, lakini nasema tusirudi kwenye vibali lakini lazima benki isaidie kuishauri Serikali kuna kitu kinaitwa *Capital Goods* na *Consumer Goods* kwa lugha ya wasomi, mmo humu wasomi mimi nilisoma kijijini mkulima tu wa kawaida. Kwa hiyo, wanasema lazima tutafsiri hapo ni kiasi gani cha fedha zetu kinaingiza matrekta na zana za kusaidia kuleta maendeleo katika sekta ya kilimo, na uendelezaji wa viwanda. Kwa sababu *experience* ya kweli inaonyesha kwamba kununua usichozalisha na kuuza ni rahisi zaidi kuliko kuhangaika kuzalisha, ndio maana utaona mkifanya hesabu kubwa katika Tanzania mtaona tunategemea sana kodi ya bidhaa tunazoingiza forodhani, sio zile tunazozalisha na ninavyoona mimi huko tunakokwenda wakubwa wanavyotutaka kutula hasa kwa utandawazi iko siku wataleta pendekezo kwamba hakuna mtu kutoza kodi ya bidhaa asizozihitaji. *(Makofi)*

Mimi nasema huko ndiko tunaelekea, utandawazi utatufikisha huko kwa sababu sisi bado tunaendelea kuwa soko la watu wakubwa na tunaamini kwamba tunapata fedha nyingi, lakini ukifanya hesabu ni fedha zinazotokana na mauzo ya forodha kwa vitu vinavyotoka nje. Unataka nirudie sasa hoja yangu niliyosema juzi kwenye semina kwamba ni hivi kwa sheria hii ya sasa na kifungu hiki kizuri ambacho kimewekwa cha kwenye hii *amendment* ukarasa ule 2(c) mimi nimeifurahia sana hii inayosema, *by inserting the phrase mortgage financing development financing lease financing* na kadha wa kadha. Sasa ndio hoja yangu ya jana inakuja kwamba Serikali na Benki Kuu ni watu wawili tu wakisha kutana wanakataa wanasema hakuna mtu kusema hadharani kwamba kilimo ni *highest riskier* wa wakopeshaji na kuiondoa hiyo lazima kuwe na mwenyewe, mwenyewe wa kilimo lazima iwe Serikali, haiwezekani mkulima akawa ndio mwenyewe, mwenyewe anayepokea fedha ziendelee kutokana na kilimo ni Serikali na Benki Kuu hawa ndio wanatakiwa wakatae hiyo na kukataa hii ni kuwa na mifuko kama hii, hii ndio inaweza kutuletea ukombozi, lakini sisi sio tu watu wenye benki ni dunia nzima. Mimi nilikwenda pia Malaysia, nimekwenda Philippines, nimekwenda nimefika Bangladesh

ambako mafanikio ni makubwa sana kwa benki ile ya akinamama ndio inaongoza dunia kwa kukopesha watu wadogo benki ya akinamama.

Lakini kilichotokea ni kwamba wanaolea hizi na wanaotoa miongozi ya namna ya kukopesha ni *Central Bank,* wanatoa kwa mfano kule kwa wenzetu wametoa muongozo, Benki Kuu inasema benki wewe utatoa *landing* kwa sekta ya kilimo ni 30% ni uamuzi wa Benki Kuu, usipokopesha 30% wanakupiga faini kwa kiwango hicho hicho wanaipa benki ambayo ilikopesha watu wakubwa. Kwa sababu tafsiri ya jambo hili ni rahisi sana benki zote tunazoziona hizi za biashara, wanatumia fedha sio zao fedha zisizokuwa zao ndio wanazo kule, kwa hiyo, ukienda wanafikiria mara mbili, tatu, wasitoe. Kwa hiyo, wanaanza kuhangaika na kuhangaika kwao kinachokuwa rahisi *cash flow* ya mnunuzi wa mahindi kutoka Sumbawanga kwenda kuuzia wenye njaa Dar es Salaam. Mnunuzi wa chumvi au wa nguo kutoka Urafiki kwenda kuuza Sumbawanga hiyo naelewa haraka sana, lakini ukianza kuzungumza habari ya mbolea, kununua maksai, kununua jembe ukalime na mvua ni ya mashaka hawaelewi.

Kwa hiyo, watu wengi sekta kubwa inayokopeshwa ni sekta ya biashara maana ndio rahisi, ya mkulima kama ya akina Mzindakaya, mimi nimetumbukia kwenye *agriculture,* nasali naomba Mungu mvua inyeshe, namshukuru Mungu imenyesha shambani na mkoa mzima angalau nitapata. Lakini ni sala, sasa utaishi utakopaje ulipe kwa hasara huyu Mungu atakusikiliza mpaka lini!

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali na Benki Kuu mkubali kuchukua kwamba suala la kilimo ni la Serikali na Benki Kuu yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu kuhusiana na uhuru wa Benki Kuu.

**NAIBU SPIKA:** Msemaji wetu wa mwisho kwa leo, sio wa mwisho kabisa, wa leo kuna wengine wengi tu wameomba na nafasi bado. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nakushuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye suala lililo mbele yetu kuhusiana na uhuru wa Benki Kuu kutenda kazi kwa uhuru zaidi katika kusimamia sera za kifedha. Katika kufanya hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yote iliyohusika na Serikali kwa ujumla, nianze kwa kusema naunga mkono hoja Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nasikiliza maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu nilijiuliza tu kama yalikuwa ni maoni ya upinzani au yalikuwa ni maoni ya upinzani Zanzibar, nilikuwa nadhani huko mbele safari ni vizuri zaidi tukawa *national* zaidi kuliko kuwa *parochial. (Makofi)*

Suala la Gavana kuwa Mwenyekiti wa Bodi lilitusumbua sana tulio wengi katika huu uhuru unaotakiwa, lakini baada ya kuangalia angalia na kufanya utundu kidogo siku

hizi ma-*internet* yanasaidia haya nimeona nchi nyingi wanafanya hivyo hata Nigeria wanafanya hivyo kwamba Gavana ndio Mwenyekiti wa Bodi. Kwa hiyo, hatuna matata nalo sana kwa upande wangu mimi, ila nilikuwa najiuliza tu kwenye Muswada wetu sijui kama ametajwa *secretary* wa hii bodi, kila nilipokuwa nikiangalia sikuweza kuona, kama yupo basi haina neno kama hayupo basi ni vizuri akaainishwa.

Katika chombo hiki cha Benki Kuu cha bodi hii na hasa viongozi, Gavana na Manaibu Gavana hawa tunahitaji watu safi kweli kweli. Tunahitaji watu safi sana sasa katika kuwapata naunga mkono kwamba Rais ndiye awateue lakini nakwenda mbali kidogo zaidi ya hapo, sio tu kwa hili, hili japo tumechelewa lakini kwa Miswada mingine itakayokuja inayohusiana na uundaji wa vyombo muhimu sana za uendeshaji wa Taifa vile ambavyo Serikali yenyewe itachambua na kuona kwamba vinafaa kuingia kwenye *category* hiyo ningeomba nafasi ya Bunge ieleweke katika vyombo hivi muhimu sana vichache vitakavyokuwa vimehainishwa na Serikali, basi itafutwe namna ambayo Bunge nalo litahusika katika kuchuja baadhi ya watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi jirani moja hapa jirani zetu kabisa yuko Waziri wa Usalama yuko matatani, yuko Gavana wa Benki Kuu yuko matatani, yuko Katibu Mkuu Wizara ya Fedha matatani, wako Makatibu Wakuu wa Wizara zingine tatu wako matatani, *deputy governors* wako matatani, kwenye *scandal* moja tu *Golden Bank.*.

Kwa hiyo, kuna umuhimu kabisa wa kuchuja watu hawa na mifano iko hapa karibu ya kikundi kidogo cha watu ambao wametia hasara nchi yao, hasara kubwa sana na sasa tunawaongezea hawa mamlaka ya kufanya mambo kwa uhuru zaidi wanavyotaka zaidi, kwa hiyo, napendekeza kwamba siku zijazo kwa Miswada mingine ya mbele ya safari Serikali yetu ijaribu kuangalia na kuorodhesha *category* fulani fulani za madaraka ya nchi hii ambapo Bunge litahusika katika kupitia pitia kabla hawajawa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13(7) Gavana na *Deputy Governors* wake ni wafanyakazi ambao ni *full time,* lakini kifungu cha 8 wanapewa tena ruhusa hasa 8(b) ya kuweza *acting* au *Directors of any Cooperation in Tanzania,* sasa nilidhani hii ni ile ambayo wazungu wanasema *is to eat your cake and one to have it.* Wabunge tumekataliwa kuingia katika *Booard of Governors* ya *Bank of Tanzania* na sababu zake zinaeleweka na mimi nakubali kabisa. Sasa wao tena ambao wako kwenye *apex regulatory board* wanataka tena kuwa Wakurugenzi kwenye vitu vingine vingine huko chini, hii italeta *conflict of interest,* mimi nilidhani wabaki pale marupurupu yao ni mazuri, kazi hii nzuri ghorofa zile mbili zilizokaa pale, ukikaa mle hali ya hewa ni nzuri huna sababu tena ya kwenda vichochoroni kuwa *director of anything.* Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hili lingetazamwa ili wabaki pale watufanyie kazi *full time* kama sheria inavyosema, wakiona kama hapatoshi basi waamue moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masuala mawili mengine ambayo ningependa kusema yenyewe ya jumla, la kwanza wenzangu wamelizungumzia na mimi niongeze kidogo *high landing rates* hatuwezi kuendelea kwa utaratibu huu na benki kuu ninyi ndio mna *supervisor* haya mambo ndio mna *regulate* haya mambo, ndio maana mabenki yanalalamika kwamba wana fedha nyingi hazikopesheki kwa Watanzania, riba yake ni

kubwa mno na wamesema wenzangu hapa, ili upate maendeleo lazima ukope, uweke lakini ukope.

Kwa hiyo, baada ya kuongezewa madaraka haya hebu jaribuni kuangalia namna gani mnaweza mkapunguza au kurekebisha hizi *landing rates* kwa nchi hiyo hiyo jirani nilikuwa nasema mwanzoni kuna Mbunge mmoja alipeleka Bungeni hoja Mheshimiwa Joh Donde na hapa wala sio kwamba haiwezekani, kwa hiyo, si vizuri sana Bunge likaanza kufanya kazi ya Benki Kuu wakati wenyewe mpo na madaraka mmeongezewa. Kwa hiyo, natumaini baada ya sheria hii kuwa imepita, mtaangalia sana masuala haya yanatuchelewesha sana Watanzania katika maendeleo.

Lingine Benki Kuu na benki nyingine hamjaweza kutufanya Watanzania tuwe na *saving culture* Watanzania wengi hawana *account* benki wala hawaweki fedha benki, wala hawajihusishi na benki, wala kukopa wala nini. Iko haja ya kuwa na mkakati maalum katika kushirikisha Watanzania katika shughuli zao na masuala ya kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la dhahabu, Benki Kuu ya nchi yoyote ile pamoja na mambo mengine hujihusisha na masuala ya dhahabu na kwa nafasi ni washauri wa Serikali katika masuala ya sera za kiuchumi na sera za kifedha. Hivi Benki Kuu mnaridhika kweli na hali ya mikataba iliyoko hivi sasa ya dhahabu nchini mwetu, je, mmeshauri nini Serikali yetu katika kuboresha suala hili, kwa sababu hii ndio moja ya rasilimali ambayo ingetusogeza sana mbele, lakini tunaibiwa hivi hivi tunaona, ndio *feeling* ya Watanzania wengi na nadhani ndio *feeling* hata ya Wabunge wengi. Sasa nilikuwa naishauri Serikali yetu kwanza *BOT* muishauri Serikali lakini vile vile na mimi nashauri hapa hebu tuwaite hawa wenye makampuni ya dhahabu, tuwaambie kwamba sisi Serikali hatuna maneno lakini wananchi wanahisi kwamba ninyi mnawaibia, ndio hisia iliyopo na kwa kweli ukitazama wanatuibia hawa watu iko haja kabisa ya kukaa chini na kurekebisha mambo haya, si vyema hata kidogo kuja nchini hapa ukachukua dhahabu yote ile ukatupatia hiyo *penalty* uliyotupatia hivi kwa nini kwanza usingekuja tu, tofauti yake ni nini hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba sana Benki Kuu iishauri Serikali na katika maeneo ya mikataba basi na nyie muwe washauri ili tupate mikataba mizuri na wachimbaji wa madeni yawe ni dhahabu na madini mengine na hapa ningependa kutoa ushauri kwa Serikali kama kuna migodi mingine mipya huenda ikaanza hivi karibuni, mimi sijui nasema tu kama iko migodi ambayo inakaribia kuanza labda au ipo kwenye *pipe line,* hiyo ingesimama kwanza mpaka turekebishe mambo yetu, ili hawa watakaoanza waanze kwa utaratibu mpya. Kwa sababu nia yetu ni kutekeleza Ilani na kuhakikisha nchi yetu inakwenda mbele na tunaamini tukirekebisha baadhi ya haya mambo tutapata pesa nyingi na tutatekeleza mambo mengi ya Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tunayo nafasi kubwa ya kujadili hoja hii, kwa hiyo, kama kuna watu wanafikiri tumefunga

orodha bado hatujafunga na hata hivyo nina orodha ya watu ambao watajadili kesho lakini na wengine pia mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja, Jumatatu tulipokuwa tunafanya kikao cha *briefing* tulieleza kwamba kuna Taasisi ambazo Wabunge wanawakilishwa, moja ilikuwa ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, Mbeya, nyingine ilikuwa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, sasa na nyingine imetokea *Tanzania Commission for Universities,* nayo ni nafasi. Kwa hiyo, kila Taasisi ni nafasi moja, moja, kwa bahati mbaya sana kwamba inabidi watakaopenda kuchukua na kugombea nafasi hizi watabidi wachukue fomu kesho asubuhi, tarehe 30 Machi, 2006 na kurudisha saa 10 kesho tarehe 30 Machi, 2006, uchaguzi utafanywa tarehe 31 Machi, 2006 mara baada ya kipindi cha Maswali na Majibu. Kwa hiyo, wale watakaopenda kuchukua nafasi katika Taasisi hizi wana muda wa kesho asubuhi tu.

Kwa hiyo, nadhani inatosha, unaenda kwa Katibu wa Bunge atawapeni fomu na mtajaza halafu saa 10.00 jioni ndio itakuwa mwisho wa kurudisha fomu. Uchaguzi utakuwa tarehe 31 Machi, 2006 saa nne asubuhi baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, nadhani nimeeleweka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.26 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 30 Machi, 2006 saa tatu asubuhi)*